# KUCHUNGUZA MASUALA YA KISIASA KATIKA RIWAYA ZA SHAABAN ROBERT: MFANO WA *KUSADIKIKA* NA *KUFIKIRIKA*

**BIBIANA MASSAWE AMBROSE**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2014**

## UTHIBITISHO

Mimi Profesa T.S.Y.M. Sengo ninathibitisha kwamba nimesoma tasinifu hii iitwayo ***Kuchunguza Masuala ya Kisiasa Katika Riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa Kusadikika na Kufikirika*** na ninapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza matakwa ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili wa sanaa (Fasihi ya Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

______________________________

Sheikh, Profesa, Daktari, T.S.Y.M SENGO

**(Msimamizi)**

______________________

Tarehe

## HAKI MILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi **Bibiana Massawe Ambrose**, ninathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

……………………………………………..

Sahihi

……………………………………………..

Tarehe

# TABARUKU

Ninapenda Kuitabaruku kazi hii kwa Mume wangu na Watoto wetu wapendwa.

## SHUKURANI

Ninawiwa shukurani nyingi na watu wengi ambao siwezi kuwataja wote katika shukurani hizi. Msaada walioutoa katika kufanikisha utafiti wangu ni mkubwa mno usiolipika hata kidogo. Wafuatao wanastahiki shukurani za pekee. Kwanza, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyenzi Mungu kwa kunipatia afya na nguvu nyingi zilizonisaidia kukamilisha kazi hii.

Pia, sina budi kumshukuru msimamizi wangu wa tasinifu hii Sheikh, Daktari, Profesa, T. S.Y.M. Sengo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala kuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Usaidizi wake haupimiki wala kulipika. Ninachoweza kusema ni asante sana mwalimu wangu Profesa Sengo, Mwenyezi Mungu akubariki na kukujaalia afya njema na maisha marefu.

Hali kadhalika ninawashukuru wataalamu wa ndani na nje ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania ambao walikuwa kutoa msaada kila wakati nilipohitajia. Ninawashukuru wazazi wangu wote wawili kwa kunizaa, kunilea, na kunisomesha hadi kufikia hatua hii ya elimu. Asanteni sana.

Ninawashukuru sana wale waliokuwa karibu nami katika kipindi chote cha masomo. Walikuwa pamoja nami katika dhiki na furaha. Wao ndio walinifanya nikawa na moyo kwamba siku moja nitamaliza masomo yangu kutokana na msaada wa maisha ya kila siku waliyonipatia. Walinipa nguvu wakati niliposikia unyonge, walinilinda nilipokaribiwa na matatizo; walinifariji nilipokuwa na shida, walinipongeza nilipofanikiwa na pia walifurahi nami nilipokuwa na furaha. Waliniongoza mpaka nikafikia hatua hii ya masomo.

Majibu ya shukurani zangu ni kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kujenga amani, mshikamano na upendo baina ya watu wa dunia. Sina njia nyingine bora ya kulipa wema wao.

# IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza masuala ya Kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa *Kusadikika* na *Kufikirika*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kutathimini masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Lengo kuu la utafiti huu limefikiwa baada ya madhumuni mahususi matatu kukamilika. Madhumuni hayo ni Kubainisha masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert, Kubainisha mchango wa Shaaban Robert katika maendeleo ya kisiasa nchini Tanzania na kuchunguza mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Shaaban Robert kusawiri masuala ya kisiasa katika *Kusadikika* na *Kufikirika*. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na uchambuzi wa kimaudhui. Mikabala wa kidhamira na kimaelezo ndio iliyotumika kuchambua data za utafiti huu.

Utafiti umebaini kuwa, masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* ni uongozi mzuri, uongozi mbaya, utii wa sheria, masuala ya jinsia na kujifunza kutoka kwa wengine. Masuala haya yanawasilishwa na Shaaban Robert kwa kutumia mbinu za kisanaa za matumizi ya methali, misemo, tashibiha, kejeli, mandhari ya kidhanaishi na wahusika bapa. Masuala ya kisiasa yanayowasilishwa na Shaaban Robert yametoa mchango mkubwa katika kuimarisha uongozi wa nchi huru ya Tanganyika na baadae Tanzania.

# YALIYOMO

Uthibitisho ...... ii

Haki Miliki ...... iii

Tamko….. ...... iv

Tabaruku ...... v

Shukurani ...... vi

Ikisiri……… ...... viii

Yaliyomo ...... ix

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ...... 1**

1.0 Usuli wa Tatizo la Utafiti ...... 1

1.1 Tamko la Tatizo la Utafiti ...... 3

1.2 Lengo kuu la Utafiti ...... 4

1.2.1 Malengo Mahususi ...... 4

1.2.2 Maswali ya Utafiti ...... 4

1.3 Umuhimu wa Utafiti ...... 5

1.4 Mipaka ya Utafiti ...... 6

1.5 Hitimishi ...... 6

**SURA YA PILI: UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ...... 7**

2.0 Utangulizi ...... 7

2.1 Kazi Tangulizi ...... 7

2.2 Maudhui katika Riwaya za Shaaban Robert ...... 7

2.3 Hitimishi ...... 18

2. 4 Mkabala wa Kinadharia ........................................ 18
2.4.1 Nadharia ya Simiotiki ........................................ 19
2.4.2 Nadharia ya Dhima na Kazi ........................................ 20
2.5 Hitimishi ........................................ 21

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................ 22**

3.0 Utangulizi ........................................ 22
3.1 Usanifu wa Utafiti ........................................ 22
3.2 Watafitiwa ........................................ 23
3.3 Usampulishaji wa Watafitiwa ........................................ 23
3.4 Vyanzo vya Data ........................................ 24
3.4.1 Data za Msingi ........................................ 24
3.4.2 Data za Upili ........................................ 24
3.5 Ukusanyaji wa Data ........................................ 25
3.5.1 Uchambuzi wa Kimaudhui ........................................ 25
3.5.2 Mbinu ya Usaili ........................................ 25
3.6 Uchambuzi wa Data ........................................ 26
3.7 Mkabala wa Kidhamira ........................................ 26
3.8 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti ........................................ 27
3.8.1 Usahihi ........................................ 27
3.8.2 Kuaminika kwa Data ........................................ 27
3.9 Maadili ya Utafiti ........................................ 28
3.10 Hitimishi ........................................ 28

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ........................................................................................ 29**

4.0 Utangulizi ........................................................................................ 29

4.1 Historia Fupi ya Maisha ya Shaaban Robert na Muhtasari wa Riwaya Teule ........................................................................................ 29

4.1.1 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data ........................................................ 30

4.1.2 Uchambuzi wa Masuala ya Kisiasa katika Riwaya teule ............................ 31

4.2 Uongozi katika Jamii ........................................................................ 31

4.2.1 Uongozi Mzuri ........................................................................................ 32

4.2.2 Uongozi Mbaya ........................................................................................ 35

4.3 Utii wa Sheria ........................................................................................ 41

4.4 Kujifunza Mambo kutoka Jamii nyingine .................................................. 49

4.5 Masuala ya Jinsia ........................................................................................ 55

4.6 Amani, Umoja na Mshikamano ................................................................... 60

4.7 Hitimishi ........................................................................................ 64

4.8 Mbinu za Kisanaa katika *Kusadikika* na *Kufikirika* .................................... 65

4.8.1 Matumizi ya Methali ................................................................................ 66

4.8.2 Matumizi ya Tashibiha ................................................................................ 68

4.8.3 Matumizi ya Kejeli ........................................................................................ 71

4.8.4 Matumizi ya Mandhari ................................................................................ 74

4.8.5 Matumizi ya Wahusika Bapa ........................................................................ 76

4.9 Hitimishi ........................................................................................ 78

**SURA YA TANO: HITIMISHI, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO ........... 80**

5.0 Utangulizi ........................................................................................ 80

5.1 Muhtasari wa Masuala ya Kisiasa katika Riwaya Zilizoteuliwa .................. 80

5.2 Muhtasari wa Mbinu za Kisanaa katika Riwaya Zilizoteuliwa .................... 83

5.3 Hitimishi ........................................................................................ 85

5.4 Mapendekezo ........................................................................................ 86

5.4.1 Mapendekezo kwa Serikali ........................................................................ 86

5.4.2 Mapendekezo kwa Wachapaji ........................................................................ 86

5.4.3 Mapendekezo kwa Wasomaji ........................................................................ 87

5.4.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadae ........................................................ 87

**MAREJELEO ........................................................................................ 88**

**VIAMBATANISHO ........................................................................................ 93**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Riwaya ya Kiswahili imepiga hatua kubwa za maendeleo katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita kufikia sasa. Maendeleo haya ni ya kifani, kimaudhui na zaidi ya yote kisanaa. Kuzuka kwa riwaya ya Kiswahili kunahusishwa sana na kipindi cha ubepari. Senkoro (1976:71-82) anasema;

> Riwaya ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kitamaduni na viwanda. Suala la ukoloni na "uvumbuzi" pia liliumba hali ambazo zilihitaji kuelezwa kwa mawanda mapana zaidi ya yale ya ngano na hadithi fupi. Hapo hapo, kuzuka kwa miji na viwanda pamoja na maendeleo ya usomaji yalifanya riwaya nyingi ziandikwe. Uchangamano wa maisha ya jamii kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi wenyewe ulizua haja ya kuwa na utanzu wa fasihi ulio na uchangamano kifani na kimaudhui. Kupanuka kwa usomaji hasa wakati wa mapinduzi ya viwanda huko Uingereza kuliwafanya waandishi waandike maandiko marefu.... Riwaya ni utanzu ambao kuzuka kwake kulifungamana na kuzuka kwa ubepari.

Maelezo haya yanatupeleka katika ukweli kwamba, riwaya ndiyo fani ya kifasihi inayoeleza mambo kwa upana zaidi kuliko kazi nyingine za fasihi. Ushairi ni utanzu wa mwanzo kabisa katika kuhakiki na kueleza juu ya maisha ya jamii. Hata hivyo, ushairi hueleza mambo kwa lugha ya mkato, mafumbo, picha, sitiari na taswira mbalimbali, hivyo wakati mwingine mwandishi hukosa uhuru wa kueleza mambo kwa undani wake. Riwaya kwa upande wake, hutoa uhuru zaidi kwa mwandishi katika kuchambua na kuihakiki jamii yake. Hii haina maana kuwa ushairi hauichambui na kuihakiki jamii. La hasha, bali ushairi hutumia lugha ambayo humfanya msomaji kufikiri zaidi pindi asomapo ndipo apate ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.

Historia ya maendeleo ya riwaya ya Kiswahili imeelezwa kwa kutumia mikondo mbalimbali kama ile ya akina Senkoro (1976), Ohly (1981), Bertoncin (1980) na Sheglov (1976) pamoja na Mlacha (1987). Hata hivyo, ni kipindi cha Shaaban Robert hasa riwaya ya Kiswahili ilipoanza kuangalia maisha ya jamii za Kiafrika. Shaaban Robert aliibuka na kazi zilizoelezea maadili na siasa katika maisha. Miongoni mwa kazi zake za mwanzo ni *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Siku ya Watenzi Wote* na *Utu Bora Mkulima* ambapo zilizungumzia ujamaa, usawa kwa watu wote na bidii kazini.

Baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961 na kuanzishwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967 kazi mbalimbali zilitungwa kuhimiza ujenzi wa jamii mpya. Na si tu kuhimiza, lakini, kueleza ni mambo yapi yaondolewe na yapi yafanyike. Kazi zinazozungumzia masuala haya ni kama vile *Kichwa Maji*, *Kuli* na *Gamba la Nyoka* kutaja kwa uchache. Kazi hizi zimesheheni simulizi mbalimbali juu ya ujenzi wa jamii mpya waliyoitamani wananchi wa Tanzania. Baadhi ya kazi hizi zilisifu Azimio kwamba lilikuwa na nia njema ya kuleta usawa na haki miongoni mwa raia. Hata hivyo, waandishi wa kazi hizo walieleza ukweli kwamba njia tuliyopitishwa na baadhi ya watumishi serikalini haikuwa sawa kwa sababu walifanya mambo mengi kujinufaisha wao wenyewe. Mawazo haya yalidhihirisha ukweli kwamba, sera ya ujamaa na kujitegemea ilikuwa nzuri na yenye tija kwa taifa lakini watendaji serikalini walishindwa kutekeleza sera hiyo kwa uzalendo. Badala yake walijiingiza katika rushwa na maslahi binafsi.

Shaaban Robert hakupata fursa ya kuandika kazi za riwaya mara baada ya uhuru kwa sababu alifariki muda mfupi baada ya kupatikana kwa uhuru mwaka 1962. Hata

hivyo, mawazo yake juu ya siasa za Ujamaa na Kujitegemea yanaonekana kutokeza katika kazi zake. Chuachua (2011) anaeleza kwamba, Shaaban Robert hakuwa mtetezi wa siasa za Ujamaa na Kujitegemea kama ilivyokuwa kwa akina Mwalimu Nyerere lakini alikuwa na mawazo kwamba maisha bora kwa kila raia yatapatikana pale tu taifa na wananchi wataishi maisha ya Kijamaa na Kujitegemea. Maelezo haya yanaonesha kwamba, Shaaban Robert alikuwa na upeo wa kuona mbali zaidi kuliko wengi kati ya waandishi wa riwaya na fasihi ya Kiswahili waliokuja baada yake. Hata hivyo, hakuna utafiti wa kina uliokwisha fanyika mpaka kufikia sasa katika kuchunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert katika ngazi ya shahada ya Uzamili. Utafiti huu umefanywa ili kuziba pengo hili la kiutafiti kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

## 1.1 Tamko la Tatizo la Utafiti

Riwaya za Shaaban Robert zimepewa hadhi kubwa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili kitaifa na kimataifa mpaka kuwafanya baadhi ya wahakiki kudai kwamba Shaaban Robert ndiye mwanzilishi wa Riwaya ya Kiswahili hasa pale alipoandika riwaya yake ya *Kusadikika* (Senkoro, 1976). Hadhi na heshima kwa riwaya hizi kumewafanya wahakiki na watafiti wengi kuzimakinikia kwa nia ya kutazama undani wa mambo yanayoelezwa katika riwaya hizo mpaka kupewa hadhi kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, wengi wa wahakiki hao kama vile Sengo (1975), Senkoro (1976), Mbughuni (1978), Senkoro (1982), Msokile (1993), Taib (2008; 2009) na Chuachua (2008; 2011) hakuna ambaye amefanya tathimini ya masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert. Badala yake wamekuwa wakigusia tu kipengele hiki katika harakati zao za kukamilisha madhumuni ya utafiti

wao. Utafiti huu ulilenga kuliziba pengo hili kwa kufanya utafiti wa kina juu ya kuchunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert kupitia riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

## 1.2 Lengo kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kutathmini masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

### 1.2.1 Malengo Mahususi

Ili kufanikisha lengo kuu la utafiti huu malengo mahususi yafuatayo yatatimizwa:

(a) Kubainisha dhamira za kisiasa zinavyojitokeza katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

(b) Kubainisha mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Shaaban Robert katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

(c) Kubainisha mchango wa riwaya teule za Shaaban Robert katika maendeleo ya masuala ya kisiasa nchini Tanzania.

### 1.2.2 Maswali ya Utafiti

(a) Ni dhamira zipi za kisiasa zinazojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Kufikirika*?

(b) Ni mbinu zipi za kisanaa zinazotumiwa na Shaaban Robert katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika*?

(c) Ni upi mchango wa riwaya teule za Shaaban Robert katika maendeleo ya masuala ya kisiasa nchini Tanzania

## 1.3 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu katika Nyanja mbalimbali kama vile za kitaaluma, kinadharia, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Tunaanza na umuhimu wa kitaaluma.

**Kitaaluma:** Utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika kuongeza marejeleo katika fasihi ya Kiswahili hususani kumhusu Shaaban Robert. Watafiti, wanafunzi, wahadhiri na wadau wengine wote wa taaluma ya fasihi ya Kiswahili watauona utafiti huu kama sehemu muhimu ya kukuza, kupanua na kuendeleza mawazo yao kuhusu riwaya na fasihi ya Kiswahili kwa ujumla wake. Watautumia utafiti huu kama rejeleo katika kazi zao mbalimbali watakazokuwa wanafanya.

**Kinadharia:** Utafiti huu utakuwa pia ni sehemu muhimu ya kukuza matumizi ya nadharia mbalimbali za uhakiki wa kifasihi. Katika utafiti huu tumetumia nadharia kadhaa ambazo kwazo wasomaji wa utafiti huu watabaini mchango wake katika kufanikisha uhakiki wa kifasihi ambao ni wa kitaaluma. Baada ya kuubaini mchango huu nao basi wanaweza kuzitumia nadharia hizi katika kufanya tahakiki mbalimbali za kazi za fasihi. Kwa kufanya hivyo, watazikuza nadharia za uhakiki wa kifasihi kwa namna moja ama nyingine.

**Kisiasa:** Utafiti huu utatoa mchango katika kuelewa mawazo ya Shaaban Robert kuhusu masuala ya kisiasa katika muktadha wa Tanganyika katika kipindi cha ukoloni na baada ya hapo ingawa hakuishi muda mrefu baada ya uhuru kupatikana. Pia utafiti huu utaonesha namna Shaaban Robert alivyokuwa na uwezo wa kuona mbalimbali kuhusu siasa na ndio maana aliweza kuzungumzia siasa za Ujamaa na Kujitegemea hata kabla ya uhuru na baada ya uhuru viongozi walianzisha siasa hizo hapa nchini.

**Kiutamaduni:** Utafiti huu utatoa mchango katika kuelewa nafasi ya utamaduni wa jamii katika maendeleo ya siasa za Tanganyika na baadae Tanzania. Ni jambo lisilopingika kwamba, utamaduni una nafasi kubwa katika maendeleo ya siasa za mahali popote pale duniani. Kupitia utafiti huu tutaona namna utamaduni wa Mtanganyika na Mtanzania ulivyosaidia katika kukuza siasa za wakati huo na hivi sasa.

## 1.4 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unajikita katika kumchunguza Shaaban Robert kama mwandishi wa kisiasa kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Tumeamua kuteua riwaya hizo mbili kwa sababu ndizo hasa zitakazoweza kujibu maswali ya utafiti wetu kwa namna iliyokusudiwa na kama ilivyokusudiwa. Vilevile, uchambuzi utakaofanywa hapa ni ule wa kifasihi na hautagusa mikabala mingine ya uchambuzi wa kisiasa. Kwa mfano, wapo wanaoweza kuchambua masuala ya kisiasa kwa kutumia mikabala ya Sayansi ya Siasa (Political Science) jambo ambalo sisi hatujaligusa.

## 1.5 Hitimishi

Sura hii imefanya uwasilishaji wa vipengele vya kiutangulizi ambavyo vinatoa picha kamili ya nini hasa kinataka kutafitiwa. Hili linathibitika kupitia vipengele vya mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, madhumuni mahususi na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Utalii wa kazi tangulizi ni daraja muhimu katika kuunganisha vipengele mbalimbali katika utafiti wa kitaaluma (Kothari, 2008). Berg (2009) anaeleza kwamba ni katika utalii wa kazi tangulizi ndipo pengo la utafiti hubainishwa na kufanyiwa utafiti na kuliziba. Hivyo basi, sura hii inatalii kazi tangulizi ambazo zinaendana na mada ya utafiti ili kubainisha pengo la kiutafiti lililoachwa na watafiti watangulizi.

## 2.1 Kazi Tangulizi

Shaaban Robert ni mwandishi anayeheshimiwa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili kutokana na umahiri wake katika utunzi wa kazi za nathari na ushairi (Njogu na Chimerah, 1999). Waliohakiki kazi zake, walifanya tahakiki zao kwa malengo mbalimbali huku malengo makuu yakiwa ni kutazama fani na maudhui katika kazi hizo. Mawazo ya wahakiki na watafiti hawa ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa kuwa yanadokeza mambo muhimu ambayo sisi tumeyatafiti. Yafuatayo ni mapitio ya kazi moja baada ya nyingine ya wahakiki na watafiti waliotafiti kazi za Shaaban Robert hususani riwaya zake.

## 2.2 Maudhui katika Riwaya za Shaaban Robert

Sengo (1975) alifanya uhakiki kuhusu maandishi ya Shaaban Robert katika kipengele cha maudhui na kueleza kwamba kazi za nguli huyu wa fasihi ni hazina kubwa katika fasihi ya Kiafrika. Miongoni mwa dhamira anazozitaja kuwa zinajitokeza katika kazi hizo ni utu bora, uungwana, ustaarabu, heshima, adabu njema, haki na kila jema. Maelezo ya Sengo (1975) hapo juu ni muafaka katika kutoa

mwelekeo na mustakabali wa utafiti wetu kutokana na kule kudokeza kwake kwamba kazi za Shaaban Robert zinazungumzia dhamira mbalimbali. Ufahamu huu wa kwamba Shaaban Robert anazungumzia dhamira zinazohusiana na siasa ni dalili tosha kuwa Shaaban Robert anazungumzia masuala ya kisiasa katika kazi zake za riwaya.

Hata hivyo, utafiti wa Sengo ulikuwa mpana sana ambapo ulitalii dhamira mbalimbali katika riwaya za Shaaban Robert. Utafiti wetu umeteua kitu kimoja tu ambacho ni kuchunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Hii imeufanya utafiti wetu kuzamia kwa undani suala moja na kuufanya kuwa madhubuti kabisa.

Mtaalamu mwingine ambaye ameandika kuhusu riwaya za Shaaban Robert ni Kezilahabi (1976) ambaye aliandika tasinifu yake yenye anuani isemayo "Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya." Katika kazi yake hii anamuelezea Shaaban Robert kama mtu mwenye tafakuri kubwa mwenye uwezo wa kueleza matatizo yanayoikumba jamii kubwa duniani na si jamii yake pekee. Shaaban Robert anaeleza juu ya athari na madhara ya ukoloni kwa nchi za Afrika na kwingineko duniani.

Maelezo yanayotolewa na Kezilahabi (1976) hapo juu yana ukweli ambao unaweza kuaminiwa kitaaluma na tunaungana mkono nayo kwa asilimia mia kwa mia. Pamoja na umuhimu mkubwa wa kazi ya Kezilahabi (1976) katika kupeleka mbele utafiti wetu, bado tunauona utafiti wake kuwa haukuwa na lengo la kuchunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert ingawa yapo baadhi ya maneno yake yanayoashiria kwamba katika riwaya za Shaaban Robert kuna utajiri mkubwa wa

masuala ya kisiasa. Hivyo basi, utafiti huu ulifanywa ili kubainisha masuala mbalimbali ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

Naye Senkoro (1976) alifanya utafiti wake na kuandika makala isemayo "Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili". Katika makala hii mwandishi anaonesha kwamba riwaya za Kiswahili zikiwemo zile za Shaaban Robert zina utajiri mkubwa wa usawiri wa masuala ya kiutamaduni katika jamii za Kiafrika. Vilevile, makala hii inamuona Shaaban Robert kama mtu aliyepinga vikali imani za Waafrika za kuabudu Miungu wengi pamoja na mizimu.

Kimsingi, utafiti wa Senkoro (1976) ni kioo cha kujitazamia ili kuona kama utafiti wetu unaweza kufikia malengo yake. Hii ni kwa sababu anamtaja Shaaban Robert kama mdau muhimu katika kuelezea maendeleo ya utamaduni wa Mtanzania. Bila shaka, mtu anayeulezea utamaduni wa jamii fulani upo uwezekano mkubwa wa kuwepo masuala ya kisiasa katika kuelezea kwake huko juu ya utamaduni. Pia, mtu anayekemea jambo fulani katika jamii kama Shaaban Robert alivyokemea Waafrika kuabudu Miungu pamoja na Mizimu ni wazi kwamba mtu huyu ana chembechembe za uanasiasa katika damu yake. Utafiti wetu umefanywa ili kubainisha ni masuala gani ya kisiasa yanayojitokeza katika kazi zake za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Tofauti na utafiti wa Senkoro (1976) ambao uligusia mambo yanayoonesha kwa ufupi kwamba katika riwaya za Shaaban Robert kunawasilishwa masuala ya kisiasa, utafiti wetu umelimakinikia suala hili kwa undani ili kubainisha masuala ya kisiasa katika riwaya teule za Shaaban Robert.

Naye Mbughuni (1978) aliandika makala juu ya uhakiki wa riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Katika uhakiki wake anaeleza kwamba, dhamira ya ujenzi wa jamii mpya

inaelezwa vizuri sana katika riwaya hizo. Hata hivyo, anatoa kauli kwamba jamii mpya inayotajwa kujengwa katika riwaya hizo ni ya kidhanaishi ambayo haiwezi kutokea katika ulimwengu halisi. Kauli hii ilipingwa vikali na Chuachua (2011) kuwa Mbughuni hakumtendea haki Shaaban Robert kwa kutoa kauli ya jumla juu ya riwaya zake kwamba ni za Kidhanaishi. Nasi pia tunaungana mkono na maoni ya Chuachua (2011) kuwa si kweli kwamba riwaya tajwa zinaeleza mambo ambayo hayawezi kutokea katika ulimwengu wa uhalisia bali zinaeleza mambo ambayo yanaweza kutokea katika maisha halisi kama zikifuatiliwa na kuzingatiwa.

Hata hivyo, tunakiri kwamba mawazo ya Mbughuni (1978) yanatoa mchango muhimu katika kupeleka mbele utafiti huu. Suala la ujenzi wa jamii mpya ni la kisiasa na bila shaka mtu yeyote anayelitoa ama kulizungumzia anakuwa aidha ni mwanasiasa au ana chembechembe za uanasiasa katika damu yake. Ufahamu huu unatufanya tuelewe kwamba, Shaaban Robert anazungumzia masuala ya kisiasa katika riwaya zake tulizoziteua.

Si hivyo tu bali pia, kauli ya Mbughuni (1978) kwamba, "riwaya za Shaaban Robert ni za kidhanaishi na zinaeleza mambo ambayo hayawezi kutekelezeka," ina mchango mkubwa katika kuelewa kuwa Shaaban Robert ni mwandishi wa masuala ya kisiasa. Ni kawaida ya viongozi wa kisiasa kueleza mambo ambayo kwa namna fulani hayawezi kutekelezeka kwa nia ya kuwavutia wapiga kura wao wawapigie kura na kuchaguliwa katika chaguzi. Swali la kujiuliza hapa ni kwamba, ni kwa vipi, kwa kuandika kidhanaishi, Shaaban Robert anajenga masuala ya kisiasa katika riwaya zake? Majibu ya swali hili ni sehemu ya utafiti huu.

Senkoro (1982) alifanya uhakiki kama ule wa Mbughuni (1978) ila yeye alihakiki riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*. Katika uhakiki wake anasema kuwa, Shaaban Robert anaeleza juu ya ujenzi wa jamii mpya yenye usawa katika jamii ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Kama alivyoona Mbughuni (1978), Senkoro (1982) naye anaeleza kwamba mbinu za ujenzi wa jamii mpya zinazoelezwa katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* ni za kidhanaishi ambazo hazitekelezeki katika ulimwengu wa uhalisia. Kwa maoni yetu tunayaona mawazo haya kuwa ni ya jumla mno kwa sababu hayajafafanua kwa kina ni sababu gani zinazofanya mbinu hizo za ujenzi wa jamii mpya kuwa ni za kidhanaishi zisizotekelezeka. Utafiti wetu umekwenda mbali zaidi na kuchunguza ni kwa kiwango gani uandishi wa kidhanaishi unaoutumiwa na Shaaban Robert katika uandishi wake unasaidia kujenga masuala ya kisiasa katika riwaya zake tulizoziteua.

Mhakiki mwingine anayezungumzia riwaya za Shaaban Robert ni Beja (1988) ambaye anaeleza kwamba, riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* ni miongoni mwa riwaya za Kiswahili zinazoeleza juu ya maudhui ya Ujamaa, sera ambayo ilitekelezwa na serikali huru ya Tanganyika. Shaaban Robert ni mtu ambaye anaonekana kuwa mwenye uwezo mkubwa wa kuona mbali, ambapo alizungumzia siasa za Ujamaa kabla hata ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika.

Kimsingi, mawazo ya Beja (1988) hapo juu yanatupatia mwanga mpana zaidi wa kumuelewa Shaaban Robert kama mwandishi wa masuala ya kisiasa. Ni mwandishi wa masuala ya kisiasa kwa sababu anatufahamisha kwamba, Shaaban Robert anazungumzia Ujamaa katika riwaya zake. Ujamaa na Kujitegemea ni siasa zilizofuatwa na Tanzania mara tu baada ya kupatikana kwa uhuru kwa minajili ya

kuimarisha maisha ya wananchi yaliyokuwa taabani kutokana na unyonyaji wa Kikoloni. Utafiti huu umekwenda mbali zaidi katika kuchunguza ni kwa vipi Shaaban Robert anazungumzia Ujamaa katika riwaya zake na kwa kufanya hivyo tukawa tumeweza kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya zake tulizoziteua.

Wafula (1989) alifanya utafiti wake juu ya matumizi ya mbinu ya Istiara katika riwaya za Shaaban Robert. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, Shaaban Robert alikuwa bingwa wa matumizi ya istiara katika kuainisha na kuelezea madhila ya serikali ya Kikoloni. Kwa mfano, anaeleza kwamba, Shaaban Robert alieleza maovu na madhila ya utawala wa Kifalme dhidi ya raia akirejelea serikali na utawala wa kikoloni (Uingereza) ili wakoloni wasije wakamuua kama utawala wa kikoloni wa Kijerumani ulivyokuwa umekusudia kufanya.

Maelezo haya yanatuonesha kwamba, Shaaban Robert anazungumzia masuala mbalimbali ya kisiasa katika riwaya zake ambapo tunamuona akizungumza kama mpinzani wa siasa za Kikoloni ambazo zilikuwa ni za ukandamizaji kwa wananchi hususani katika unyonyaji wa rasilimali zao. Ufahamu huu unatufanya tufanye utafiti wa kina wenye nia ya kubainisha masuala mbalimbali ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert tulizoziteua na kisha kujibu maswali ya utafiti wetu.

Msokile (1993) alichambua fani na maudhui katika riwaya ya *Kusadikika*. Katika uchambuzi wake amegusia dhamira zinazojitokeza katika riwaya hizo huku ile ya ujenzi wa jamii mpya ikitamalaki. Tofauti na watangulizi wake tuliowaona hapo juu

yeye hakuzungumza kwamba mbinu za ujenzi wa jamii mpya zinazoelezwa katika riwaya tajwa ni za kidhanaishi. Yeye anaziona mbinu za utawala bora, utu wa mwanadamu, mapinduzi katika jamii, haki na usawa wa mwanadamu kuwa ni mbinu muafaka katika ujenzi wa jamii mpya. Kwa hili tunakubaliana naye kwa asilimia mia kwa mia na kwamba mawazo yake yanatoa mchango muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu.

Maelezo ya Msokile (1993) hapo juu yanatufanya tumfahamu Shaaban Robert kama mwanaharakati wa haki na usawa wa mwanadamu kupitia maandishi yake aliyoyaandika. Ufahamu huu unatufanya tujiulize maswali ya kwamba, kwa kufanya hivyo Shaaban Robert anaeleza masuala gani ya kisiasa? Ni katika kujiuliza swali kama hili, ndio maana utafiti huu ukafanywa ili kupata muktadha mzima wa utokezaji wa masuala ya kisiasa katika riwaya zake tatu tulizoziteua.

Mbatiah (1999) alifanya utafiti wake juu ya maendeleo katika riwaya ya kiuhalisia katika Kiswahili. Pamoja na mambo mengine alijikita katika kutoa maana haswa ya riwaya na kujikuta akitoa hitimishi kwamba, Riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* si riwaya bali ni masimulizi ya kidhanaishi na riwaya pekee za Shaaban Robert ni *Utu Bora Mkulima* na *Siku ya Watenzi Wote*. Mawazo ya Mbatiah (1999) yanatoa mchango muhimu wa kusukuma mbele utafiti wetu. Hata hivyo, hatukubaliani na maelezo kwamba *Kusadikika* na *Kufikirika* si riwaya bali ni masimulizi tu ya kidhanaishi. Kwa maoni yetu riwaya tajwa zina sifa muafaka za kuzifanya kuitwa riwaya za Kiswahili na hakuna haja ya kuzirejelea sifa hizo za riwaya katika muktadha huu.

Tunasema, hatukubaliani na mawazo yake kwa sababu ni katika riwaya hizo ambazo yeye anaziona kuwa si riwaya ndimo ambapo Shaaban Robert anajinasibisha zaidi na masuala ya kisiasa jambo linalotuvutia kuchunguza ni kwa kiwango gani tutamuita mwandishi huyu kuwa ni wa masuala ya kisiasa. Kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* Shaaban Robert anazungumzia masuala yanayofichua maovu ya Wakoloni dhidi ya raia ambayo kwa mtazamo wetu haya ni masuala ya kisiasa. Ni kwa vipi masuala haya ya kisiasa yanajitokeza katika riwaya teule ni sehemu ya utafiti wetu huu.

Mong'eri (2000) alifanya utafiti wenye lengo la kutazama maadili katika riwaya za Shaaban Robert. Katika maelezo yake inaonekana kwamba kuna maadili ya aina tatu ambayo ni ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo yanajitokeza katika riwaya za Shaaban Robert. Maelezo haya yanaonesha kutoa mchango muhimu wa kusukuma mbele utafiti wetu. Maadili ya kisiasa kuonekana katika kazi za Shaaban Robert ni ushahidi tosha kwamba Shaaban Robert ni mwandishi wa masuala ya kisiasa. Ingawa uhakiki wa Mong'eri haukuwa na lengo la kumtazama ama kumuelezea Shaaban Robert kama mwandishi wa masuala ya kisiasa lakini amedokeza jambo ambalo linasukuma mbele utafiti wetu. Utafiti wetu umekwenda mbali zaidi katika kuonesha ni kwa vipi Shaaban Robert anaelezea masuala ya kisiasa kutokana na kuandika kwake maadili ya kisiasa katika riwaya zake. Tumelifanya hili kwa kutumia riwaya zake tulizoziteua.

Naye mwanataalimu Tangoh (2008) alifanya utafiti uliokuwa na madhumuni ya kuhakiki namna Shaaban Robert alivyoshughulikia dhamira zinazomtetea mwanamke katika riwaya za Shaaban Robert. Utafiti huu umetusaidia kuelewa

kwamba, Shaaban Robert ni mtetezi wa haki za watu wote katika jamii. Kwa kufanya hivyo, anakuwa ni mtu ambaye anaheshimu na kuthamini utu wa mwanadamu. Si hivyo tu bali pia, Shaaban Robert anaonekana kuwa ni mwandishi mwenye kuona mbali zaidi kutokana na kuandikia mambo ya uanaharakati wa kumkomboa mwanamke jambo ambalo lilikuja kupata mashiko katika miaka ya 1980 takribani miaka ishirini baada ya kifo chake. Jambo hili kwa wakati huu limevaliwa njuga na kushikiliwa na wanasiasa mbalimbali mpaka kufikia wanawake kupatiwa nafasi za upendeleo katika vyombo vya maamuzi kama vile bunge, baraza la madiwani na katika nafasi mbalimbali za utumishi wa umma na ule wa binafsi. Mawazo ya Shaaban Robert kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii yanatufanya tumuone Shaaban Robert kama mwandishi anayeandika masuala ya kisiasa katika riwaya zake na hivyo kupata msukumo wa kulishughulikia suala hili katika riwaya tulizoziteua ili kukamilisha malengo ya utafiti wetu.

Pia, Chuachua (2008) alifanya utafiti juu ya taswira katika riwaya za Shaaban Robert na kugundua kwamba, Shaaban Robert ni bingwa wa kutumia taswira katika kujenga dhamira mbalimbali katika riwaya zake. Taswira ni kipengele kimojawapo kati ya vipengele vingi vya tamathali za usemi zinazotumiwa katika kuwasilisha dhamira za kazi za kifasihi. Shaaban Robert ni mwandishi mashuhuri katika utumizi wa vipengele vya tamathali za usemi mojawapo ikiwa ni taswira. Katika utafiti wetu tumelenga pia kuzitazama mbinu za kisanaa zikiwemo taswira katika riwaya za Shaaban Robert ili tuweze kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya zake tulizoziteua.

Vilevile, Taib (2008) alifanya utafiti katika kazi za fasihi ambazo zinaeleza maudhui ya dini ya Kiislamu na kupendekeza kwamba kazi hizo zinapaswa kuhakikiwa kwa kutumia mkabala wa Kiislamu kuliko kutumia mikabala ya Kimagharibi ambayo inaonekana kupotosha kazi husika pale inapotumiwa katika kuzihakiki kazi hizo. Miongoni mwa kazi alizozitaja kuwa zinaeleza maudhui ya Kiislamu ni zile za Shaaban Robert. Ni jambo lisilopingika, kwamba Shaaban Robert anazungumzia masuala ya dini katika riwaya zake. Maelezo haya yanasukuma mbele utafiti wetu kwa kuwa yanaeleza jambo ambalo linatufanya tujiulize maswali kadhaa: Kwanza, katika kuzungumza kwake masuala ya dini katika riwaya zake, anazungumza kama nani? Mwanasiasa? Shehe? Au mtu wa kawaida? Maswali haya yalitupatia hima ya kumtafiti Shaaban Robert kama mwandishi wa masuala ya kisiasa ili tuweze kuyajibu kama inavyopasa. Hivyo basi, utafiti huu ulifanywa kwa lengo la kuchunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert tulizoziteua.

Taib (2009) alifanya uchambuzi juu ya "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi." Katika uchambuzi wake anadai kwamba, Shaaban Robert anaongozwa na falsafa za utu wema, siasa na dini. Kimsingi, tunakubaliana na uchambuzi wa Taib kwa asilimia mia kwa mia kwamba Shaaban Robert aliongozwa na falsafa hizo katika utunzi wa riwaya zake. Hata hivyo, kwa maoni yetu tunaona kwamba falsafa ya utu wema ndiyo inayotawala katika kazi zake kuliko falsafa nyingine zote. Mawazo haya yanatupatia uelewa kwamba, Shaaban Robert ni mwandishi wa falsafa ya aina gani jambo ambalo linatuashiria pia kwamba Shaaban Robert anaweza kuwa mwandishi wa masuala ya kisiasa katika riwaya zake. Tunasema hivi kwa sababu, wanafalsafa huandika kuhusu masuala yanayohusu siasa.

Hivyo basi, utafiti wetu ulifanywa ili kuweza kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert ambazo tumeziteua.

Vilevile, Chuachua na wenzie (2009) walifanya utafiti juu ya riwaya za Shaaban Robert na kubainisha kwamba riwaya zake zinapinga utawala wa Kikoloni. Shaaban Robert anaonesha namna Wakoloni wanavyowanyonya na kuwagandamiza wananchi pamoja na rasilimali zao na hivyo kuwataka wananchi kupigania haki zao za msingi ikiwemo kumuondoa mkoloni nchini. Mawazo ya Chuachua na wenzie (2009) ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa sababu yamedokeza juu ya ukoloni uliokuwa ukipigwa vita na Shaaban Robert. Shaaban Robert alipiga vita ukoloni kwa sababu ulikuwa ni aina ya utawala uliokwenda kinyume na misingi ya utu wa mwanadamu. Jambo hili linathibitisha kwamba, Shaaban Robert ni mwandishi ambaye anawasilisha masuala ya kisiasa katika riwaya zake. Utafiti huu ulifanywa ili kubainisha vipengele vya masuala ya kisiasa vinavyojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert tulizoziteua.

Chuachua (2011) alifanya utafiti kuhusu "Itikadi katika riwaya za Shaaba Robert" na kubainisha itikadi ambazo zilimuongoza Shaaban Robert katika utunzi wa riwaya zake. Miongoni mwa itikadi zilizomuongoza nguli huyu katika utunzi wake ni ile ya Kisoshalisti iliyoasisiwa na Mrusi Karl Marx. Kwa kuongozwa na itikadi ya aina hii katika utunzi wa riwaya zake ni dhahiri kwamba, Shaaban Robert ni mtu anayejali na kuheshimu utu wa mwanadamu. Tunalazimika kusema hivyo kwa sababu, itikadi ya Kisoshalisti inasisitiza kwa kiasi kikubwa wanadamu wote waishi kwa kuthamini na kuheshimu utu wa mwanadamu.

Mawazo haya yanaonesha kwamba, Shaaban Robert ni mwandishi wa masuala ya kisiasa kwa sababu inaonekana bayana itikadi zake zikimpeleka huko. Hata hivyo, uchunguzi wa masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert halijajadiliwa katika utafiti wa Chuachua (2011) kwa sababu halikuwa sehemu ya madhumuni yake. Utafiti huu umefanywa ili kubainisha kinaganaga ni masuala gani ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya za Shaaban Robert tulizoziteua.

## 2.3 Hitimishi

Sura hii imepitia machapisho ya kazi tangulizi kumuhusu Shaaban Robert na kufanikiwa kubainisha pengo la utafiti ambalo litashughulikiwa katika utafiti wetu. Wengi wa watangulizi hawa wanaonekana kugusia kwamba Shaaban Robert anazungumzia masuala ya kisiasa katika riwaya zake. Hata hivyo, inaonesha kwamba, watafiti hawa watangulizi walizungumzia hoja hiyo kwamba Shaaban Robert anazungumzia masuala ya kisiasa katika riwaya zake kama sehemu tu ya kukamilisha malengo ya utafiti na tahakiki zao. Utafiti huu unafanywa ili kuchunguza kwa kina masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

## 2. 4 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni muongozo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli fulani kufanikiwa kama ilivyokusudiwa. Kwa mfano, katika kufanya utafiti wa kitaaluma ni wajibu kwa mtafiti kuongozwa na nadharia maalumu katika kufanya utafiti wake ili kuufanya utafiti ufanikiwe vizuri na uaminike. Utafiti huu utaongozwa na nadharia za Simiotiki na Dhima na Kazi. Maelezo ya kina kwa kila nadharia yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

### 2.4.1 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuhakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Wamitila, 2002:132).

Ishara zinazojitokeza katika kazi za fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Chandler (1992) anaeleza kwamba, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa alama hizo. Wasomaji na watazamaji wa kazi za fasihi hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama hizo. Mawazo haya yanakamilishwa na yale ya Chandler (1992) aliposema kuwa, tunafikiri kwa kutumia alama. Alama hizo zinakuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na mtenda au yambwa. Anaendelea kueleza kwamba, kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kama kirejelee, yaani kinasimama kwa niaba ya kitu kingine badala ya chenyewe.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja (a signifier), yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejelee (a signified), yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja, na kirejelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao.

Barthes (1994) akaja na aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa Kimatukio, Kihemenitiki, Kiseme, Kiishara na Kiurejelezi.

Shaaban Robert kama ilivyo kwa baadhi ya waandishi wengine anatunga riwaya zake kwa kutumia lugha ya picha, ishara, mafumbo, sitiari, na taswira kali haswahaswa. Nadharia ya Simiotiki itatoa mwongozo muafaka katika kuzichambua aina zote hizo za matumizi ya lugha na kisha kuwezesha kufanikisha madhumuni ya utafiti huu. Nadharia nyingine ni ile ya Dhima na kazi, nayo inaelezwa kama ifuatavyo:

### 2.4.2 Nadharia ya Dhima na Kazi

Nadharia ya Dhima na Kazi imeasisiwa na Sengo (2009). Nadharia hii inazichambua kazi za fasihi kwa kuangalia kazi na dhima kwa kila kipengele cha fasihi. Mwanafalsafa huyu anaendelea kueleza kwamba, kila kitu katika kazi ya fasihi kimetumiwa kwa dhima maalumu katika kazi husika. Kwa mfano, hata waandishi wanapoteua majina ya vitabu vyao hufanya hivyo kwa madhumuni mahususi. Mawazo haya tunakubaliana nayo na tunayaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na kwamba yanasukuma mbele utafiti wetu. Yanasukuma mbele utafiti huu kwa sababu ili kuweza kubainisha masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert ni lazima tuchunguze matumizi ya vipengele mbalimbali vya kifani katika riwaya tulizoziteua kwa sababu vimetumiwa kwa madhumuni mahususi ya kujenga dhamira mbalimbali. Kwa mfano, *Kusadikika* ambalo ni jina la kitabu limetumiwa kwa dhima maalumu ambayo tukiichunguza vizuri tunaweza kuelewa mambo mengi ambayo yatadhihirisha masuala mbalimbali ya kisiasa katika riwaya teule.

## 2.5 Hitimishi

Nadharia zilizowasilishwa katika sura hii ni muafaka katika kukamilisha madhumuni ya utafiti wetu. Nadharia hizo zinatoa mwongozo kamili katika uchambuzi wa data za utafiti huu kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Kwa mfano, kupitia nadharia ya Simiotiki tumeweza kuchambua methali, tashibiha, misemo na kejeli zilizotumika katika riwaya za Shaaban Robert ambazo tumeziteua ili kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Utafiti ni sayansi ambayo hufanywa kwa kuongozwa na taratibu maalumu ambazo mwisho wa siku zikifuatwa vizuri hutoa matokeo stahiki pasipo upendeleo wowote (Babbie, 1999). Taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika kufanya utafiti zinaitwa mbinu za utafiti. Hivyo basi, sura hii inawasilisha mbinu zitakazotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Mbinu hizo ni pamoja na usanifu wa utafiti, populesheni, sampuli, usampulishaji, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data

## 3.1 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu utatumia mbinu ya usanifu ijulikanayo kama uchunguzi kifani katika kukusanya data. Yin (1994) anasema kwamba, uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambayo mtafiti huteua sehemu au jambo au kitu maalumu ambacho atakifanyia utafiti kati ya vingi vilivyopo ili aweze kukidhi mahitaji ya utafiti wake. Katika utafiti huu, riwaya za Shaaban Robert ndizo zilizoteuliwa na kufanyiwa utafiti katika kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza. Mbinu hii ya usanifu ni muafaka katika utafiti huu kwa sababu inatoa fursa kwa mtafiti kulitafiti jambo moja kwa muda wa kutosha na hivyo kupata majibu sahihi ya maswali ya utafiti wake (Robson, 2007). Vilevile, mbinu hii humuwezesha mtafiti kuzama na kulitafiti jambo moja kwa undani kabisa na kisha kulitolea mahitimishi stahiki (Cresswel, 2009). Isack na Michael (1981) wanasema kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuufanya utafiti wake kwa gharama nafuu.

### 3.2 Watafitiwa

Kimsingi ili mtafiti aandike tasinifu yake anahitajika kuwa na data za kumuwezesha kufanya hivyo. Data za utafiti hazipatikani mahali pengine ila kutoka kwa watafitiwa. Kwa mantiki hiyo basi, watafitiwa ni jumla ya watu au vitu ambavyo ndivyo hasa humpatia mtafiti data za utafiti wake. Katika utafiti huu kutakuwa na watafitiwa watu na vitu. Kwa upande wa watu, ni familia, marafiki pamoja na ndugu na jamaa wa Shaaban Robert ambao jumla yao ni 20 ndio hasa walikuwa watafitiwa katika utafiti huu. Kwa upande wa vitafitiwa, jumla ya vitabu viwili vya Shaaban Robert vilitafitwa. Vitabu hivyo ni *Kusadikika* na *Kufikirika*.

### 3.3 Usampulishaji wa Watafitiwa

Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa katika kundi kubwa na kuwa ndio wakilishi wa kundi hilo lote (Keys, 1980). Sampuli Lengwa na Nasibu ndizo zitakazotumika katika kufanikisha ukusanyaji wa data. Sampuli Lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huiteua akiwa na imani kwamba, itampatia data itakayowezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake (Newman na Wenzake, 2006:22). Kwa msingi huu basi, sampuli lengwa hapa ni riwaya za Shaaban Robert ambazo tumekwisha kuzitaja hapo awali pamoja na wanafasihi, familia, ndugu na jamaa wa Shaaban Robert. Mtafiti ameteua kazi hizi kwa kuwa anaamini kwamba, zitampatia majibu ya maswali yake ya utafiti. Vilevile, Sampuli Nasibu nayo imetumika katika utafiti huu ambapo hii ni aina ya sampuli ambayo hutoa fursa sawa kwa watafitiwa wote kuchaguliwa ili kutoa data za utafiti kama ilivyokusudiwa na mtafiti (Babbie, 1999). Sampuli Nasibu imetumika katika kukusanya data kutoka katika riwaya husika. Pale mtafiti alipobaini msitari au aya katika riwaya teuliwa

kuwa inaelezea masuala ya kisiasa aliinukuu katika daftari maalumu la kukusanyia data kwa ajili ya uchambuzi wa data za utafiti wake.

### 3.4 Vyanzo vya Data

Utafiti huu umekusanya data za msingi na za upili kupitia vyanzo mbalimbali kama vinavyoainishwa hapa chini.

#### 3.4.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huo anaoufanya sasa (Kothari, 1992:95). Hivyo basi, data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Vilevile, data za msingi zilikusanywa kutoka kwa wataalamu wa fasihi, familia, ndugu jamaa na marafiki wa Shaaban Robert ambao jumla yao ni 20.

#### 3.4.2 Data za Upili

Tofauti na data za msingi, data za upili ni zile ambazo tayari zimekwisha kukusanywa na watafiti wengine na kuchapishwa katika ripoti, makala, tasinifu, magazeti na vitabu. Hii ni mbinu ya kukusanyia data mezani, yaani mtafiti haendi maskanini kuhoji au kufanya mahojiano na watafitiwa. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa katika maktaba kuu ya Taifa, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Taasisi ya Taaluma za Maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Baada ya mtafiti kuainisha vyanzo vya data atakavyovitumia katika utafiti wake, jambo linalofuata ni ukusanyaji wa data kutoka katika vyanzo alivyoviainisha. Hivyo basi, ukusanyaji wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu zifuatazo:

### 3.5.1 Uchambuzi wa Kimaudhui

Uchambuzi wa Kimaudhui ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo humpatia mtafiti data baada ya yeye ama msaidizi wake kusoma matini iliyoteuliwa kwa kina. Kutokana na kusoma huko ndipo pale akutanapo na sehemu inayohusiana na malengo yake ya utafiti na kuinukuu katika shajara maalumu (Kothari, 2008).

Mbinu hii ilitumika katika kukusanya data za msingi na data za upili. Katika ukusanyaji wa data za msingi mtafiti na msaidizi wake waliandaa shajara ambalo lilikuwa na vichwa/mada zinazohusiana na malengo ya utafiti ama kile kilichokusudiwa kukusanywa. Baada ya hapo walianza kusoma riwaya teuliwa kama zilivyoainishwa hapo juu na kila walipoona sentensi au aya katika riwaya hizo inayohusiana na madhumuni ya utafiti waliinukuu katika shajara.

### 3.5.2 Mbinu ya Usaili

Miongoni mwa mbinu maarufu za ukusanyaji wa data ni usaili (Babbie, 1999). Kothari (2008) anaeleza kwamba, usaili ni mbinu ya utafiti ambapo utafiti humkutanisha mtafiti na watafitiwa wake ana kwa ana na kufanya mazungumzo yanayohusiana na utafiti wake kwa lengo la kupata data za utafiti. Kupitia mbinu hii mtafiti aliandaa maswali ambayo aliwauliza watafitiwa wake katika usaili aliofanya nao. Watafitiwa waliosailiwa ni familia ya Shaaban Robert, marafiki pamoja na

ndugu zake wa karibu ambao jumla yao ni 20. Matumizi ya mbinu hii ni muafaka katika utafiti huu kwa sababu ilimpatia mtafiti data za uhakika kwa kutumia muda mfupi na gharama nafuu.

### 3.6 Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa zisingewezi kuwa na maana yoyote mpaka zitakapochambuliwa na kuwasilishwa katika tasinifu. Vilevile, data hizo hazichambuliwi kienyeji kienyeji tu bali pia kuna mbinu muafaka ambazo zinapaswa kufuatwa kadiri zitakavyokuwa zimeteuliwa. Mbinu iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu ni ile ya uchambuzi wa kimaelezo. John (1997) anaeleza kwamba, uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma shairi, kisha kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo wake na kadhalika. Mbinu hii pia huhusisha uchambuzi wa lugha iliyotumika. Kwa kufanya hivyo, mbinu hii huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo iliwezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

### 3.7 Mkabala wa Kidhamira

Kazi ya fasihi ina sifa ya kuchambuliwa kwa kutumia mikabala mbalimbali ya kifasihi kulingana na lengo la mhakiki. Mkabala wa Kidhamira ni mojawapo ya mikabala maarufu katika uhakiki wa kazi za kifasihi. Maelezo haya yanathibitishwa na Taylor na Broad (1984), Benner (1985) na Leininger (1985) kama wanavyonukuliwa na Aronson (1992). Aronson (1992) anaeleza kwamba, mkabala wa kidhamira hutumika kuichambua kazi ya fasihi kwa kuzingatia hatua kuu nne. Hatua ya kwanza ni ya kukusanya data, hatua ya pili ni kuoanisha mada na data

husika (kubainisha data zinazohusaina na mada ya utafiti). Hatua ya tatu ni kupangilia data kwa namna ya kuoanisha dhamira kuu na dongondogo. Hatua ya nne ni kuandaa hoja au nyanja zitakazozingatiwa katika uchambuzi wa dhamira baada ya kusoma ama kupitia machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti husika. Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia hatua zote nne za uchambuzi wa data kama zilivyoainishwa hapo juu.

## 3.8 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

### 3.8.1 Usahihi

Usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika (Cohen, na wenzake, 2000). Usahihi wa data katika utafiti huu utadhibitiwa kwa mbinu mbili za ukusanyaji wa data ambazo ni uchambuzi wa kimaudhui na usaili. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kidhamira na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ndizo zitakazotumika katika kukusanyia data, Usahihi wa mbinu hizi unatokana na ukweli kwamba mapungufu ya kila moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine.

Vilevile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake na wanataalimu wa fasihi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

### 3.8.2 Kuaminika kwa Data

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa/kuzalisha matokeo yaleyale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zilezile (Kothari, 2008). Kuaminika kwa data hujitokeza pale ambapo kunakuwa na

uhusiano ama ulingano katika taarifa zilizotolewa na watu walewale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikiwa kwa kutumia mbinu mbili za kukusanyia data na nadharia mbili (Simiotiki na Dhima na Kazi) za uhakiki wa kifasihi.

## 3.9 Maadili ya Utafiti

Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa kuzingatia mtafiti ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo basi, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti wetu ulikuwa ni wa uwandani na maktabani tulihakikisha kuwa madondoo kutoka katika riwaya teuliwa yanadondolewa kwa usahihi na kufanyiwa uchambuzi wa kifasihi kwa kuongozwa na nadharia mbili (Simiotiki na Dhima na Kazi) za uhakiki wa kifasihi.

## 3.10 Hitimishi

Sura hii imewasilisha mbinu za utafiti ambazo zilitumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wetu. Mbinu hizo zinajumuisha zile za maskanini na maktabani. Mbinu za maktaba zinahusisha ukusanyaji wa data kwa kusoma kwa makini kazi zinazohusiana na mada ya utafiti huu ili kupata data za kujazilizia data za msingi. Vile vile, data za msingi zilikusanywa kwa kusoma kwa makini riwaya teule ili kupata data zinazoonesha kwamba Shaaban Robert ni mwandishi wa masuala ya kisiasa. Kwa upande mwingine data za msingi zilikusanywa kwa kufanya usaili na watu wa karibu wa Shaaban Robert wakiwemo wanafamila, ndugu, jamaa na marafiki.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti ili kutimiza madhumuni mahususi na hatimaye lengo kuu la utafiti. Kabla ya kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti tunaanza kwa kutoa muhtasari wa historia ya Shaaban Robert na riwaya zake mbili tulizozishughulikia.

## 4.1 Historia Fupi ya Maisha ya Shaaban Robert na Muhtasari wa Riwaya Teule

Shaaban Robert alizaliwa tarehe 1 mwezi wa kwanza mwaka 1909. Shaaban Robert alianza shule mwaka 1922 na kumaliza 1926 katika shule ya Kichwele ambayo kwa sasa inafahamika kama Uhuru Mchanganyiko. Alipenda sana kusoma na kujiendeleza kielimu lakini jitihada zake hazikuzaa matunda kwa haraka kwa sababu ziliporwa na wakoloni kwa lengo la kumtumia kama chombo cha kutawalia. Hata hivyo mwaka 1932 aliendelea na masomo kwa njia ya posta ambapo mwaka 1934 alitunukiwa Diploma ya Fasihi. Mwaka 1936-37 alitunukiwa cheti cha *English Level*. Ni dhahiri kuwa Shaaban Robert alikuwa ni mtu mwenye juhudi kubwa katika kujiendeleza kielimu na kama si wakoloni angalifika katika ngazi za juu zaidi.

Ilipofika mwaka 1926 alianza kazi katika idara ya Forodha Tanga. Hapo alidumu kwa miaka takribani 18. Mwaka 1944-1946 alihamishiwa Idara ya Wanyamapori huko Mpwapwa. Mwaka 1946 alirudishwa Tanga na kuwa Afisa Ardhi wa jimbo la Tanga. Aidha barua zake zinaonesha pia aliwahi kufanya kazi katika mikoa ya

Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam na Kisiju. Shaaban Robert alifariki tarehe 20.6.1964 na kuzikwa huko Vibambani tarehe 21.6.1962.

Shaaban Robert ameandika kazi za fasihi zipatazo ishirini na nne. Miongoni mwa kazi zake ni *Kusadikika* na *Kufikirika* tulizozitafiti katika utafiti huu. *Kufikirika* ni riwaya iliyotunga mwaka 1946. Ni miongoni mwa riwaya zilizojengwa na picha zenye mafumbo mazito. *Kufikirika* ni riwaya ngumu kiasi kueleweka. Hii ni kwa sababu usimulizi wa vitushi vyake ni tata. Ni riwaya inayoeleza mambo ya kufikirika mawazoni mwa mtu na hayapo katika ulimwengu halisia. Riwaya hii inazungumzia udhalimu ambao usingeweza kutajwa waziwazi. Hili linadhihirishwa na maelezo ya mtunzi katika sehemu ya utangulizi ambapo anatujengea taswira ya nchi ya Kufikirika. Lengo lake ni kujitanibu na mikono mirefu ya serikali ya kikoloni.

*Kusadikika* ni riwaya iliyotungwa mwaka 1948 na kuchapishwa mwaka 1951. Riwaya hii ni pacha wa Kufikirika. Kusadikika ni jina lililotumika kurejelea tafsiri ya neno sadiki lenye maana ya amini. Kwa hiyo, Kusadikika maana yake ni kuaminika. Maudhui yanayochimuza katika kazi hii yanadhihirisha kuwa, jina hili halikutumika kwa mtazamo chanya, bali ni kiudakuzi. Utawala wenye taasubi za kikoloni, wa kusadikika, unadakuliwa na mwandishi kwa kuonesha waziwazi ghaidhi aliyonayo dhidi yake.

### 4.1.1 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti umefanywa kwa kuongozwa na madhumuni na maswali yake ya utafiti. Lengo mahususi la kwanza lilihusu kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Lengo mahususi la pili lilihusu kubainisha mbinu za kisanaa

zinazotumiwa na Shaaban Robert katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Lengo mahususi la tatu lilihusu kutathmini mchango wa riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* katika maendeleo ya siasa nchini Tanzania. Kutokana na ukaribu wa kimantiki wa dhumuni mahususi la kwanza na la pili tukaona ni vema yaunganishwe katika uwasilishaji, uchambuzi na mjadala. Ufuatao ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

### 4.1.2 Uchambuzi wa Masuala ya Kisiasa katika Riwaya teule

Masuala ya kisiasa ni miongoni mwa mambo yanayojenga dhamira kuu katika kazi za fasihi ya Kiswahili na nyinginezo duniani. Omary (2011) anaeleza kuwa, siasa ya jamii husika ndiyo huamua aina ya mfumo wa maisha ambayo itafuatwa na wanajamii wake. Ni katika siasa ndipo sera, mipango, bajeti na maamuzi kuhusu miradi ya maendeleo hutolewa na kuletwa mbele ya wananchi kwa ajili ya utekelezaji. Hii ni sawasawa na kusema kuwa masuala ya kisiasa ndiyo huongoza masuala ya uchumi, utamaduni na kijamii kwa kiasi kikubwa. Siasa ndiyo hujenga uongozi na mfumo wa utawala katika jamii. Mpangala (2007) anaeleza kuwa siasa ndiyo inayoamua wapi barabara ijengwe na inajengwa, wapi zahanati ijengwe na inajengwa, wapi shule ijengwe na inajengwa na kinyume cha haya pia huamuliwa na siasa. Shaaban Robert katika riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika* ameeleza masuala mbalimbali ya kisiasa ambayo yana umuhimu mkubwa katika maendeleo ya mataifa machanga kama ilivyo Tanzania. Masuala hayo ni:

## 4.2 Uongozi katika Jamii

Uongozi katika jamii ni kitu ambacho kimekuwapo tangu pale mwanadamu wa kwanza alipoumbwa. Adam na Hawa ndiyo wanadamu wa kwanza kuumbwa na

Mwenyezi Mungu ndipo uzazi wao ukafanya jamii kubwa iliyopo leo. Hii ni kwa mujibu wa mafundisho ya dini ya Kiislamu na Kikristo- dini zenye wafuasi wengi duniani. Adamu ndiye alikuwa kiongozi wa Hawa katika kipindi chao wao wawili tu na baadaye wakapata watoto na watoto nao wakazaana na kufanya umma mkubwa. Kitendo cha watu wawili tu walioumbwa mwanzo kuwa na uongozi wao ni ishara kuwa, uongozi ni kitu muhimu mno katika maendeleo ya mwanadamu. Uongozi ndiyo unaotoa dira na mwelekeo wa maendeleo katika jamii. Hivyo kila jamii inapaswa kuwa na uongozi wake bila kujali idadi ya watu iliyonayo. Hata hivyo, si kila uongozi una nia ya kuleta maendeleo kwa watu wake licha ya kuwa sababu ya kuanzishwa kwake ni hiyo. Hapa tunapata aina kadha za uongozi; uongozi mzuri, uongozi mbaya, uongozi wa mabavu na uongozi wa upendeleo. Aina hizi za uongozi zinapatikana katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

### 4.2.1 Uongozi Mzuri

Nyerere (1967) anaeleza kuwa, uongozi mzuri ni ule ambao nia yake kuu ni kuwaletea wananchi maendeleo kupitia sera na mipango mizuri. Sera na mipango hiyo mizuri, hutokana na wananchi wenyewe na kazi ya serikali ni kusimamia na kuwezesha wananchi kuandaa sera na mipango mizuri ya maendeleo. Hili litafikiwa kama serikali itakuwa imeandaa namna bora za kuwafanya wananchi wake kuwa weledi katika fani mbalimbali za ustadi katika maisha. Mawazo kama haya yalikwishatolewa na Shaaban Robert katika *Kusadikika* pale aliposema:

> *Serikali ya Kufikirika ililazimisha sana ustadi wa watu wake katika kazi zake. Kwa hivi Wafikirika waliidilika katika njia nyingi sana. Nchi ilikuwa ina serikali imara, waongozi wa ubongo mzuri, mahakimu wa haki, waandishi bora, wanachuoni mufti, wasafiri na wagunduzi wavumilivu na wajasiri, mabaharia wa moyo mkuu na wenye kuthubutu na askari wa miili migumu, mishipa minene, kano*

> *kavu zenye nguvu na shabaha nzuri. Watu wa adili katika kila mwendo wa maisha. Naam, watu wote walijipambanua katika kazi zao. Matendo kwao yalikuwa ni halali na kujigamba bure ilikuwa ni haramu. Mavuno na mapato mbalimbali ya watu wa kufikirika yalikuwa hayana kifani hata kidogo kwa ubora katika ulimwengu (uk. 17).*

Huu ni uthibitisho kuwa uongozi mzuri lazima uhakikishe watu wake wanakuwa wataalamu na wajuzi katika fani zote za maendeleo. Hii ndiyo njia pekee ya kujiletea maendeleo. Maendeleo huletwa na watu wenyewe na si wageni au serikali bila ya jitihada za kila mtu katika jamii. Shaaban Robert anazitaka serikali kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapatiwa elimu ili kutokana na elimu hiyo aweze kuisaidia familia na nchi yake kupata maendeleo. Pia inaonyeshwa kuwa, uongozi mzuri ni ule unaohamasisha watu wake kujibidiisha katika kufanya kazi bila kuchoka na kutumia muda mwingi kufanya kazi badala ya kujigamba na kujisifu kwa maneno tu. Waswahili husema, "maneno matupu hayavunji mfupa" na "mkono mtupu haulambwi." Hii inathibitisha kuwa uongozi mzuri ni chachu ya maendeleo kwa jamii yoyote ile yenye nia na dhamira ya kufanikiwa.

Dondoo hili linadai kuwa, nchi haiwezi kuwa na maendeleo kama uongozi haujahakikisha kuna watafiti na wagunduzi wabobezi katika nchi yao. Watafiti na wagunduzi ndio ambao hutafuta masuluhisho ya changamoto za maisha na kuzisahihisha na kusonga mbele kimaendeleo. Kwa hiyo, ni wajibu wa serikali makini kuwekeza vya kutosha katika eneo la utafiti na ugunduzi kwa matokeo makubwa. Katika uhalisia hali imekuwa sivyo, uwekezaji katika utafiti na ugunduzi umekuwa hafifu kadri siku zinavyokwenda na hivyo kurudisha nyuma maendeleo. Mpangala (2007) anaulaumu uongozi kwa kutotoa kipaumbele cha uwekekezaji wa

bajeti ya serikali katika utafiti na ugunduzi kwani kinarudisha nyuma maendeleo. Anaeleza kuwa, nchi zilizoendelea zimefika hapo zilipofika kutokana na uwekezaji mkubwa katika utafiti na ugunduzi. Sekta hii ndiyo inayosaidia nchi hizo kubuni bidhaa mpya, huduma mpya na mbinu mpya katika uzalishaji viwandani na katika kilimo. Kutokana na kubuni bidhaa na mbinu hizo mpya imekuwa kazi rahisi kwa mataifa hayo kumiliki soko huria na kpata faida kubwa ya kuwapatia utajiri. Kinyume chake, bidhaa za mataifa maskini huwa hazina ubora unaoweza kufikia ule wa nchi zilizoendelea na kukosa nafasi katika soko huria.

Katika *Kusadikika* pia kunasawiriwa dhamira ya uongozi mzuri ambao unapenda kusikiliza maoni ya wananchi wake kabla ya kuwachukulia hatua yoyote ile. Hii inaonesha kuwa, uongozi upo kwa ajili ya watu na hauko madarakani kwa ajili ya kujiamulia mambo yenye masilahi kwao. Mtunzi anasema:

> *Mfalme hakuona sababu ya haraka ya kulikata shauri la mshitakiwa. Kwa hivi, alisema kuwa mshitakiwa alitaka muda wa siku sita ili atimize kazi iliyotakiwa na baraza hili. Hakutaka kutolewa katika gereza. Yumo katika gereza na atakuwa katika hali hiyo mpaka mwisho wa maelezo yake. Maelezo yatakayopatikana kwake yatakuwa faida ya baraza. Muda huu ukiisha, hukumu inayostahili itatolewa kwa mshitakiwa. Wakati una mabawa kama ndege. Uvumilivu ukitumiwa siku sita ni sawa na saa sita. Kwa kuwa haifai kuonekana kuwa baraza haina saburi, haja ya mshitakiwa ya muda wa kueleza sababu za kuanzisha uanasheria katika nchi hii haina budi kukubaliwa. Hili liliposemwa baraza liliahirishwa (uk. 10).*

Maelezo haya yanaonesha namna uongozi wa mfalme ulivyokuwa sikivu kwa watu wake hasa pale walipokuwa na haja ya msingi ya kusikilizwa. Hii ni ishara ya uongozi mzuri katika jamii kwa kuwa kila mtu ana haki sawa ya kusikilizwa hoja yake au maombi yake bila kipingamizi chochote. Baadhi ya wajumbe wa baraza hasa Majivuno, hakuwa tayari kuona ombi la mshitakiwa likikubaliwa na hivi alitaka

aadhibiwe haraka iwezekanavyo. Hata hivyo, uongozi mzuri wa mfalme ulisikiliza maombi ya mshitakuwa na kukubaliwa kwa muda ule ule alioomba bila ya kupunguzwa. Huu nao ni ushahidi wa uongozi mzuri unaopaswa kuigwa na jamii zote duniani. Mpangala (2007) anafafanua kwamba, uongozi wa aina hii hupatikana katika nchi zenye utawala wa Demokrasia na si katika nchi za Kidikteta kama zilivyo nchi nyingi za Afrika. Hivyo, uandishi huu wa Shaaban Robert ni wito kwa watawala wa nchi za Kiafrika na kokote duniani ambako Demokrasia yao inalegalega kuiga na kutekeleza. Kitendo cha wananchi kusikilizwa na uongozi wao, huwapa faraja ya kujiona kuwa wao ni bora na bila wao basi uongozi huo usingelikuwapo. Wananchi wanauona uongozi kuwa ni mali yao na si mali ya kiongozi au viongozi.

### 4.2.2 Uongozi Mbaya

Aina nyingine ya uongozi iliyopo katika riwaya teule za Shaaban Robert ni uongozi mbaya. Hii ni aina ya uongozi ambayo, kuwapo kwake uongozini si kwa manufaa ya wananchi wake bali watu wachache tu ukiwapo uongozi huo. Uongozi wa aina hii huongozwa na tamaa ya kujilimbikizia mali na kusahau kuwa mali hiyo inatokana na rasilimali za wananchi na hivyo ilipasa kuwanufaisha wananchi wote. Wakati wa kuandikwa kwa riwaya za Shaaban Robert ilikuwa ni kipindi ambacho watawala wengi walikuwa wakijilimbikizia mali na kuwasahau wananchi ambao ndio wachumaji wa mali hiyo kupitia kodi na ushuru unaotozwa na serikali. Hali hiyo haijabadilika sana kwani hata siku hizi wapo viongozi ambao kazi yao ni kujilimbikizia mali. Mbaya zaidi, mali hizo huhifadhiwa katika nchi za nje ili isijulikane kuwa kiongozi fulani ana mali nyingi. Tazama mfano kutoka katika *Kufikirika*:

> *Nina mali katika hazina inayoweza kununua kitu chochote kinachopatikana kwa thamani kubwa katika soko za dunia bila ya kuonyesha upungufu. Hazina hizo zimejaa tele fedha, dhahabu, almasi, yakuti, zumaridi, feruzi na kila namna nyingine ya vito vya thamani bora. Mashimo ya chuma, pua, shaba, bati, madini nyingine na makaa. Ghala za nafaka, meno ya tembo, pembe za faru, ambary, sandarusi, pamba, hariri, manyoya, sufi, katani, ngozi, nta, ng'amba, zari, ubani, mashanga, vioo, majora ya nguo kila namna, chumvi, sukari, mafuta, vileo na bidhaa nyingi nyingine mbalimbali. Ng'ombe, farasi, nyumbu, punda, kondoo, mbuzi na wanyama wengine ambao mazizi yao hayahesabiki katika nchi… (uk.02).*

Huu ni mfano wa utajiri alionao kiongozi hali ya kuwa kuna mwananchi ambaye hajui hata atakula nini kwa siku hiyo. Tabia ya viongozi kujilimbikizia mali kwa kiasi hiki ni ishara ya tamaa na kutojali watu wengine. Hii ni tamaa kwa sababu, mtu mmoja hahitaji mali nyingi kiasi hicho ili aishi. Mali hizi ni zaidi ya kipimo cha juu kabisa cha mahitaji ya mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Hali hii ipo katika maisha halisia ya siku hizi ambapo viongozi hawaridhiki na mapato makubwa wapatayo kupitia marupurupu na mishahara na kufanya vitendo vya rushwa ili kujilimbikizia mali. Kwa mfano katika nchi ya Tanzania, kumekuwa na malalamiko kila siku juu ya viongozi kushiriki katika vitendo vya rushwa ili kujitajirisha. Tuhuma za *External Payment Arreas* (EPA), RICHMOND na *Independent Power Tanzania Limited* (IPTL) zimewahusisha viongozi wa serikali kukwapua fedha nyingi kinyume cha sheria. Baadhi ya viongozi hao wamedhihirika kuwa na fedha nyingi katika mabenki ya nje ya nchi zilizopatikana kwa njia zisizo halali. Hata mmoja kati ya viongozi hao alikiri kuwa ni kweli ana kiasi cha fedha nje ya nchi ila ni vijisenti vidogo tu. Fedha zilizoitwa kuwa ni vjisenti zinakadiriwa kuzidi shilling billion moja za Tanzania (Omary, 2012).

Uongozi wa mabavu ambao huamua mambo bila ya kuwashirikisha wananchi unasawiriwa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* za Shaaban Robert. Uongozi wa aina hii husahau kuwa madaraka waliyonayo ni ya wananchi na si yao. Wakati wowote wananchi wanaweza kuchukua madaraka yao. Viongozi hawa hufanya maamuzi kwa mabavu kwa nia ya kujineemesha na kujitajirisha. Uongozi wa aina hii umekuwapo katika nchi nyingi za Afrika katika kipindi cha Ukoloni na baada ya kupata Uhuru (Ngware, 1998). Mpangala (2007) anasema kuwa, utawala wa mabavu ambao hujulikana kama utawala wa Kidikteta umesababisha nchi nyingi za Afrika kuingia katika mapigano ya wenyewe kwa wenyewe kila mara na kusababisha mauaji ya wananchi wake. Utawala wa aina hii ni urithi kutoka serikali za Kikoloni. Mpangala (ametajwa) anatoa mfano wa mgogoro unaoendelea katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda umesababishwa na kuwapo utawala wa mabavu katika nchi hizo. Katika *Kufikirika* kunasawiriwa utawala wa mabavu, kwa mfano:

> *Mbiu maalumu ilitangaza habari kwa watu kuwa waganga wote walitakiwa na serikali ya kufikirika. Upesi kama iwezekanavyo watu hao lazima wafike kwa mfalme Mtukufu wa Kufikirika. Mtu yeyote mweledi wa dawa, utabiri au dawa akikosa kutii wito wa Mfalme Mtukufu bila udhuru mwema lazima atahukumiwa uhalifu na kutotii amri ya Serikali wakati wa jambo kubwa la taifa na la haraka lililotaka msaada wa kila mganga. Mtu asiyehudhuria lakini akiweza kujitetea katika mashtaka kwa sababu za kutosha kama vile ugonjwa na mambo mengine ambayo hayaepeki Serikali itamsamehe; lakini akishindwa kufanya hivyo na ikiwa itathibitika kuwa ni mhalifu hasira ya mfalme mtukufu wa Kufikirika itakuwa juu yake pasipo huruma. Waganga wote walitakiwa wakutane kwa Mfalme Mtukufu baada ya siku thelethini za tangazo (Uk. 04).*

Hapa inaoneshwa kuwa, kiongozi wa nchi alipatwa na shida ambayo ilihitaji msaada kutoka kwa wananchi wake ili itatuliwe. Shida yenyewe ilikuwa ni ugumba wa Mfalme na utasa wa Malkia. Hii ni shida au tatizo ambalo linaweza kumpata mtu

yeyote katika jamii na kuhitajia msaada ni kitu sahali kabisa. Hata hivyo, tangazo la serikali kuwataka waganga kuitika wito wa Mfalme linaonesha kuwa ni la mabavu, la amri na siyo la utashi wa waganga hao. Huu ni ubabe na ubavu wa serikali dhidi ya raia wake. Suala la kumpatia mtu matibabu hufanikiwa kama tabibu atakuwa ametuliza akili yake na asifanye kazi ya utabibu kwa kushurutishwa. Matokeo ya utawala wa mabavu husababisha hasara kubwa kwa serikali na kwa wananchi pia. Kutokana na ubabe wa Mfalme Mtukufu kutaka kutibiwa kwa mabavu kulimsababishia kupoteza mali nyingi kabla ya kupata mtoto.

Tangazo la serikali juu ya matibabu ya Mfalme Mtukufu pamoja na Malkia limefanywa kwa amri na kwa haraka mno ili kuhakikisha kuwa wanapata mtoto. Hii ni tafauti na mtu wa kawaida anapokuwa na tatizo ambalo lilihitaji msaada wa serikali kupatiwa kwa wakati na haraka kama ilivyo kwa Mfalme. Katika jamii ya leo viongozi wengi wa serikali hutibiwa nje ya nchi kwa fedha nyingi za serikali huku wananchi wa kawaida wakikosa huduma za msingi za afya katika maeneo yao. Mambo haya hufanyika kutokana na ubabe wa serikali wa kuamua mambo bila kuwashirikisha wananchi na kuwataka watekeleze kwa lazima. Imani yetu ni kuwa kama serikali ingewashirikisha wananchi katika kuamua juu ya viongozi kutibiwa nje ya nchi wananchi wasingekubali.

Vile vile, maelezo ya Shaaban Robert yaliyonukuliwa hapo juu yanasawiri kitaswira utawala wa Kikoloni uliotawala nchi nyingi za Afrika. Utawala wa Kikoloni ulitoa huduma muhimu za maisha ya mwanadamu kwa taabu mno katika maeneo machache huku maeneo mengi yakiachwa bila ya huduma yoyote. Maeneo yaliyopatiwa huduma kiduchu ni yale ambayo yalizalisha mali ghafi zilizohitajika katika viwanda

huko Ulaya. Maeneo mengine ambayo yalitoa wafanyikazi wa kuzalisha mali ghafi hizo hawakupatiwa huduma kabisa. Jambo hili linaendelea hata leo ambapo maeneo yakaliwayo na viongozi na yale ya mijini ndiyo yanayopatiwa huduma muhimu kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na maeneo ya vijijini. Watu wa vijijini ndiyo huzalisha chakula kinacholiwa na viongozi pamoja na watu wa mijini. Hivi ni kusema kuwa watu wa kijijini hukidhi haja za viongozi na watu wa mijini lakini viongozi hawakidhi haja za watu wa vijijini. Iqbali Shaaban Robert, anasema:

> *Baba yangu alikuwa ni mtu aliyejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuona mbali. Siku moja nikiwa ninazungumza naye nilimuuliza swali; hivi baba ulifikiria nini hata ukaandika riwaya zako za Kusadikika na Kufikirika? Jibu lake lilikuwa kama ifuatavyo: Mwanangu mpendwa, niliandika kazi hizi katika kipindi cha utawala wa Kikoloni na mengi yaliyosemwa humu yaliwalenga wakoloni na yataendelea kuwalenga viongozi watakaofuata baada ya Ukoloni. Viongozi hawa ni wale wasiojali raia wao, hufanya maamuzi kwa mabavu tena maamuzi ambayo ni yenye maslahi kwao na si kwa wananchi wote. Hivyo niliona nchi hizi niziite Kusadikika na Kufikirika ili asije mtu kunishika shati kuwa nimemtaja yeye (Iqbal Shaaban Robert, 20/08/13).*

Maelezo haya yanathibitisha kuwa *Kusadikika* na *Kufikirika* ni riwaya ambazo zinasawiri masuala ya siasa katika jamii ya kipindi cha Ukoloni na ile ya sasa. Viongozi wengi wa leo wanafanya maamuzi ambayo yanawanufaisha wao wenyewe na kuwasahau Watanzania wenzao. Uingiaji wa mikataba mibovu unaofanywa na serikali na Wawekezaji ni ishara tosha ya maamuzi ya kibabe yenye masilahi kwa viongozi. Mikataba mingi inayoingiwa ni ile ambayo huwapatia wawekezaji faida kubwa na serikali hupata kidogo sawasawa na hakuna kitu.

Dhamira ya utawala wa mabavu na ubabe inapatikana pia katika *Kusadikika*. Dhamira hii inajitokeza katika kazi hizi mbili kutokana na ukubwa wa athari zake kwa jamii. Katika *Kusadikika* kunasemwa:

> *Sheria za Wasadikika zilikuwa hazimwamuru mshitakiwa kujitetea juu ya ushahidi wa mshitaki. Aghalabu mashtaka mengi yalikubaliwa bila ya swali wala kiapo. Labda hii ndiyo sababu ya nchi yao kuitwa kusadikika. Kama mashtaka yaliletwa mbele ya baraza na wafalme, watoto wao, matajiri au watu wengine maarufu nguvu ya desturi hii ilifanywa maradufu. Hapana shaka kuwa salama ya watu wadogo ilikuwa kidogo sana katika nchi hii. Lakini mashtaka juu ya uanasheria yalikuwa na habari ngeni kabisa. Wasadikika walikuwa bado kusikia utaalamu huu. Kwa hamu kubwa ya kutaka kujua maana yake, baraza ilitamani mshitakiwa kuamriwa kueleza maana ya uanasheria kabla ya hukumu kufanywa (Uk. 07).*

Kitendo cha mshitakiwa kuhukumiwa bila ya kusikilizwa ni ishara kuu ya uvunjaji wa haki za binadamu popote pale duniani. Sheria kama hizi huwekwa na viongozi ili kuzuia watu wasipinge maamuzi na maelekezo yatakayotolewa na viongozi hao juu ya jambo lolote lile katika jamii yao. Dondoo linaonesha mashaka juu ya hatma ya watu wadogo; yaani watu wa kawaida katika jamii. Watu hawa wataishia kunyanyaswa kila siku kwa sababu huogopa kwenda kinyume na fikira za watala na kutopewa nafasi ya kujitetea na kupata hukumu za vifungo magerezani. Utawala wa mabavu huweka daraja kubwa baina yake na wananchi ambao ndiyo huwaweka madarakani viongozi hao. Sheria bora za kutawala nchi hutakiwa kutokana na wananchi wenyewe na siyo viongozi kukaa chini na kuunda sheria kandamizi na za unyanyasaji kwa wananchi. Kwa mfano, sheria nyingi zinazotawala katika nchi nyingi za Afrika ni urithi kutoka serikali za Kikoloni ambazo ni kandamizi kwa wananchi.

Kimsingi, nchi kadhaa, Tanzania ikiwamo, zipo katika harakati za kutunga katiba mpya zitokanazo na wananchi wenyewe. Hata hivyo, baadhi ya viongozi waliopo madarakani hawako tayari kuona mamlaka makubwa waliyoachiwa na Wakoloni yanarudi kwa wananchi. Kwa kawaida madaraka huwa yana raha na pumbazo kwa

baadhi ya viongozi. Kutokana na hali hii, si rahisi kwa nchi hizi kuweza kuwa na katiba zitokanazo na wananchi na tawala za mabavu zitaendelea kushika hatamu za uongozi katika nchi nyingi za Afrika.

### 4.3 Utii wa Sheria

Sheria hutungwa na wanadamu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wananchi wote bila uonevu wa aina yoyote. Katika jamii kuna watu wenye nguvu na wengine wasio na nguvu, kuna walemavu na wasio walemavu, kuna matajiri na masikini, kuna wanaume na wanawake na kwa jumla kuna makundi mbalimbali ya watu na kila kundi lina haki zake za msingi. Ila kila kundi kati ya haya ili liweze kupata haki zake ni lazima pawepo sheria na kila mmoja awajibike kuzitii sheria hizo. Sheria za kila jamii hutokana na makubaliano baina ya wanajamii wote na kama si wote basi walio wengi. Huanza kwa kuandaliwa katiba ambayo ndiyo sheria mama na sheria nyingine zote hutokana na katiba. Baada ya katika kuwapo sheria nyingine zote hutungwa na Bunge chombo kilicho na dhamana ya kufanya kazi hiyo katika jamii nyingi duniani. Katika nchi ya Kufikirika kulikuwa na baraza ambalo kazi yake ni kutunga sheria na kila mwananchi alipaswa kutii sheria hizo. Mtunzi anasema:

> *Hapakuwa na mtu aliyeweza kuvunja sheria pasipo kupatilizwa. Wafikirika walihesabu kuvunjwa sheria kuwa si uhalifu mkubwa tu lakini ni dhambi vile vile iliyostahili laana. Sheria zao zilikuwa imara kama zilivyowezekana kufanywa. Zilikuwa si sheria dhaifu au halisi kama uzi wa buibui ambao hukatwa na nzi mkubwa na kunasa nzi mdogo tu. Imara ya sheria hizo ilikuwa mbele ya kila mtu pasipo mapendeleo; mkubwa kwa mdogo, mnguvu kwa mnyonge; na tajiri kwa masikini. Hata mfalme hakuweza kutenda dhara bila ya kulaumiwa na sheria. Kwa sheria kama hizi Kufikirika ilikuwa ni nchi ya salama kwa raia, na ya fahari kwa mfalme aliyeitawala; lakini watu pengine hukutana na majaribu au huchafukiwa na mambo hata wakaiishi katika nchi ya salama na fahari (Uk. 31).*

Maelezo haya yanaonesha namna sheria ilivyokuwa msumeno katika nchi ya Kufikirika. Udhibiti wa sheria huwafanya wananchi kuwa makini na mambo ambayo yatawasababishia kuvunja sheria za nchi. Hii ilitokana na umadhubuti wa serikali ya nchi hiyo kumchukulia hatua kila aliyevunja sheria husika. Dondoo linaonesha kuwa hata kiongozi mkuu wa nchi hawezi kuamua kufanya jambo lolote kinyume na sheria eti kwa sababu yeye ni kiongozi. Maneno haya yalikuwa ni kebehi na kejeli kwa serikali ya kikoloni ambayo ilifanya mambo kinyume na sheria. Serikali ya kikoloni iliwanyang'anya wananchi mashamba yao kwa nguvu, wananchi walilipishwa kodi kwa lazima, walifanyishwa kazi katika mashamba ya mkonge, chai, kahawa na pamba kwa lazima na malipo kidogo na waliopinga waliuawa kikatili kabisa. Shaaban Robert anapoandika kuwa hata kiongozi wa nchi hiyo alikuwa muumini mkubwa wa kutii sheria za nchi ilikuwa ni njia mojawapo ya kuchochea jamii ya Watanganyika kwa wakati huo kudai Uhuru wao kwa nguvu.

Nukuu iliyotolewa hapo juu inatoa maelezo kuwa katika nchi ya Kufikirika watu wote walikuwa sawasawa mbele ya sheria. Kiongozi hakuweza kutumia mamlaka ya uongozi wake kufanya mambo yaliyopingana na sheria bila ya kuchukuliwa hatua ya aina yoyote. Mtu tajiri hakuweza kutumia utajiri wake kuvunja sheria dhidi ya watu wengine ambao ni masikini. Maelezo haya ni kejeli juu ya watu wa jamii iliyopo hivi sasa. Matajiri na baadhi ya viongozi huvunja sheria za nchi kwa makusudi ya kujinufaisha wao wenyewe bila ya kuchukuliwa hatua zaidi. Ipo mifano hai ya viongozi kushiriki katika rushwa lakini viongozi hao huhamishwa au husimamishwa kazi bila ya kupelekwa katika vyombo vya sheria kupatiwa stahili yao.

Pia, nukuu hii inaonesha kuwa mtu aliyevunja sheria katika nchi ya Kufikirika alifanya makosa makubwa yasiyoweza kusamehewa na wanajamii wenzake. Anasema: "Wafikirika walihesabu kuvunjwa sheria kuwa si uhalifu mkubwa tu lakini ni dhambi vile vile iliyostahili laana." Hii inaonesha kuwa kuvunjwa sheria ni kitu kisichovumilika katika jamii ya Wafikirika. Katika jamii ya leo kuvunja sheria ni jambo la kawaida na mvunjaji wa sheria hupata sifa kutoka kwa baadhi ya wanajamii. Kwa mfano, wafanyakazi wanaofanya kazi katika mamlaka au sekta za fedha hutarajiwa kuiba fedha kinyume cha sheria na kupata utajiri. Mtumishi wa mamlaka ya mapato kwa mfano akistaafu kazi bila ya kuwa na fedha nyingi za kumtosha kuwa tajiri baadhi ya wanajamii humlaumu kuwa si mjanja. Kitendo hiki kimeenea karibu kila sekta na kuonekana kuwa ni cha kawaida hali ya kuwa ni uvunjifu wa sheria za nchi. Kwa maelezo ya Shaaban Robert, jamii ni lazima ibadilike na kuheshimu na kutii sheria za nchi kwa sababu ndizo zisababishazo kuwapo kwa amani na usalama kwa raia wote.

Katika riwaya ya *Kusadikika* nako kunasawiriwa masuala ya utii wa sheria kwa wananchi wake wote bila upendeleo na umahususi. Sheria zikifuatwa vizuri bila ya kupuuzwa hata kidogo duniani kutakuwa ni mahali bora pa kuishi. Shaaban Robert anasema:

> *Zamani za marejeo yake hapa, alisema habari za mamlaka ya kiasi, heshima iliyo na wastani, uhuru wa kadri, na nguvu yenye mpaka. Mtu mwenye mamlaka ya kiasi hawatesi watu walio chini ya mamlaka yake wala hajitesi yeye mwenyewe; mwenye heshima iliyo ya wastani hujiheshimu yeye mwenyewe na wengine; mwenye uhuru wa kadiri ni muungwana yeye mwenyewe na wengine; na mwenye nguvu yenye mpaka hadhulumu wala yeye hadhulumiwi. Mambo manne haya ni mbegu za mimea ya mazao ya hali njema, mapatano, ustawi na amani duniani. Mbegu hizi zililetwa hapa kutoka mbali kwa kusudi la kupandwa katika ardhi ya Kusadikika. Kwa kupandwa*

> *katika ardhi ilikusudiwa kuwa mambo haya yakizoezwa katika mioyo ya watu matokeo mfawadha yatakuwako katika maisha yao. Kabuli hakutazamia kuwa watu watafaidiwa na mazao yake tu, lakini alitumaini vile vile chini ya vivuli vya matawi ya mimea hii watesaji na wateswa watapumzika na watakane nasaha kwa mapenzi na furaha (Uk. 25).*

Nukuu hii inaeleza umuhimu wa utawala wa sheria katika kuwafanya watu wote wenye mamlaka na madaraka kuyatumia kwa kiasi. Mamlaka huweza kumlewesha aliyekabidhiwa mamlaka hayo na akafikia kuwaangamiza wale walio chini yake bila hatia yoyote. Mamlaka humpatia mtu kiburi na dharau kwa wale anaowatawala. Hali hii humfanya awatese watu wengine na kujitesa yeye mwenyewe pia. Mtu anapowatesa watu hujitesa naye mwenyewe kwa sababu dhambi ya dhuluma ya haki ya mtu huwa haipotei na daima humrudia mambo mabaya yule mwenye kudhulumu. Shaaban Robert anafafanua kuwa kiongozi au mtu yeyote anapokuwa na mamlaka ya kiasi, heshima iliyo ya wastani, mwenye nguvu yenye mpaka na mwenye uhuru wa kadiri huwa ni mtu mwenye amani daima na huishi maisha mazuri. Mambo haya yanaweza kupatikana kama zikiwepo sheria maridhawa na kila mtu akazitii na kuziheshimu sheria hizo. Hivyo, kupatikana kwa mambo hayo katika jamii kutategemea utii wa sheria kwa viongozi na wananchi kwa pamoja.

Hata hivyo, katika dondoo hili Shaaban Robert anatumia falsafa ya hali ya juu kuukebehi utawala wa Kikoloni na tawala nyingine ambazo zimefuata baada ya Ukoloni. Serikali hizi zimekuwa ni za mabavu na uonevu kwa raia ambapo kiongozi anakuwa hana ukomo wa mamlaka. Kiongozi katika kipindi cha Ukoloni aliweza kuamka asubuhi na kuamrisha mtu fulani auwawe au aondoke mahali fulani aende akaishi mahala pengine mara moja. Mtu huyo aliuwawa au kuhama na maelekezo ya

kiongozi yakatimia. Katika kipindi cha hivi karibuni, vyama vya upinzani katika siasa vimekuwa vikilalamika kuwa watawala wa nchi wamekuwa na mamlaka makubwa ambayo yanawafanya kuwa Mungu watu. Kutokana na hali hiyo wamekuwa wakidai nchi hizi zitunge katiba mpya ambayo itawezesha kupunguzwa kwa mamlaka ya wakuu wa nchi na kuyarudisha mamlaka makubwa kwa wananchi wenyewe. Baadhi ya nchi za Afrika zimefanikiwa kutunga katiba mpya na nyingine zipo katika harakati za kukamilisha upatikanaji wa katiba mpya.

Mzee Sharif Khatibu ambaye alikuwa rafiki wa karibu wa marehemu Shaaban Robert alitueleza kuwa:

> *Kila mara Shaaban Robert alikuwa akizungumza juu ya utawala wa kikoloni kuwa ulichukua mamlaka kubwa ya kuamua mambo bila ya kuwashirikisha wananchi katika nchi yao. Wakoloni waliweza kuua raia bila huruma kwa madai kuwa raia huyo au hao wamepingana na sheria za unyanyasaji za utawala wa Kikoloni (Sharif Khatibu, 16/08/2013).*

Nchini Tanzania kwa mfano, wameanza kutekeleza ushauri wa Shaaban Robert miaka zaidi ya hamsini baadaye. Shaaban Robert aliiona hali ya watawala kuwa na mamlaka kubwa ya kupindukia tangu siku nyingi lakini watawala hawakuwa tayari kufanya hivyo mpaka msukumo mkubwa ulipotoka kwa viongozi wa vyama vya upinzani na kwa wananchi. Mfano mzuri wa mamlaka kubwa kwa viongozi unatolewa na Shaaban Robert katika *Kusadikika*. Anasema:

> *Juu ya kuwachinja mahabusu kwa kuua, mjumbe wetu alisikia kuwa adhabu kama hiyo ilitumiwa sana zamani katika Ardhi. Wakati huo mashtaka yalikuwa hayachujwi. Mchujo wa mashtaka ulipohalalishwa katika sheria zao, mambo yalibadilika sana. Baadhi ya watu walituhumiwa kuwa walikuwa wahalifu walionekana kwa kuyachuja mashtaka yao, kuwa walikuwa si wahalifu kamwe. Walisingiziwa bure. Jambo hili lilipunguza sana machinjio ya washtakiwa. Adhabu ya kifo ilikusudiwa kubatilishwa katika sheria*

> *za Ardhi mara watu wake walikoma kuuwana wenyewe. Bidii ya kuwafunza watu jinsi ya kutendeana wenyewe ilianza siku nyingi huko. Kila mtu alijitahidi kupingana na majaribu mabaya kwa nguvu zake zote. Hapana shaka Ardhi itakuwa mahala bora kwa maisha ya watu (Uk. 46).*

Mamlaka makubwa kwa viongozi huwafanya kuamua jambo lolote hata kama linahatarisha maisha ya watu katika jamii. Inaelezwa kuwa watu waliuawa pasipo mashtaka yao kusikilizwa na kutazamwa kama yalikuwa kweli au hawakutenda na bila ajizi walihukumiwa hukumu nzito za kifo. Hata hivyo, baada ya kutungwa sheria za kutaka mashtaka ya washukiwa kuchujwa wengi wao walionekana kutokuwa na hatia na kuachiwa huru. Hili liliwezekana baada ya kutungwa sheria na watu wote kutia shime kutekeleza sheria hiyo. Shaaban Robert anatumia lugha ya kiungeushi kwa kueleza kuwa katika Ardhi ndiko kulikokuwa na sheria kandamizi huko zamani. Sasa hivi katika ardhi mambo yanatakiwa kuwa ya haki na si kunyanyasa watu. Huu ni ukengeushi kwani yanayosemwa hapa yalikuwa yakifanyika katika ardhi hiyo hiyo ila tu kwa sababu nchi aliyoiandikia ni ya angani. Hapa alikuwa anailenga serikali ya Kikoloni kwa kuwa ndiyo ilikuwa ikifanya mambo ya uvunjivu wa sheria kwa wananchi wa Tanganyika na kwingineko kuliko tawaliwa.

Kimsingi, wanaosemwa hapa si Wakoloni peke yao bali hata viongozi wa sasa pamoja na raia wasioheshimu utawala wa sheria. Katika nchi nyingi za Afrika bado wapo baadhi ya viongozi na raia wanaojihusisha katika vitendo vya uvunjivu wa sheria na mauaji ya raia wasiokuwa na hatia. Hii yote hufanyika kutokana na ukweli kuwa baadhi ya viongozi hao hutaka kuwa na mamlaka makubwa na kuendelea kutawala bila kupingwa kwa upande mmoja. Kwa upande wa pili ni wapinzani na

waasi wasiokubaliana na utawala usio adilifu nao kuanzisha vita vya kupingana na utawala huo. Katika vita hivyo watu wasio na hatia kama akina mama, watoto na watu wazima hupoteza maisha.

Kutokana na umuhimu wa kuheshimu utawala wa sheria, Shaaban Robert anatumia lugha ya kuhamasisha wananchi kutii sheria za nchi. Katika sehemu ya mwisho ya dondoo hili anasema, "Kila mtu alijitahidi kupingana na majaribu mabaya kwa nguvu zake zote. Hapana shaka Ardhi itakuwa mahali bora kwa maisha ya watu." Huu ni uhamasishaji kwa raia kuhakikisha kuwa wanatii sheria za nchi kwa bidii zote ili wasikutwe na hatia na hatimaye wakahukumiwa kwa mujibu wa sheria. Uhamasishaji huu unaofanywa na Shaaban Robert ni wa kisiasa na kidini vile vile. Ni katika majukwaa ya kisiasa ndipo wanasiasa huwahubiria wananchi kutii na kuheshimu sheria za nchi na mamlaka yake. Kwa muktadha huu, Shaaban Robert anazungumzia masuala ya kisiasa katika *Kusadikika*. Kwa upande wa pili anazungumzia juu ya mafundisho ya dini ambayo humtaka kila mwanadamu kuwa mtu mwema na kutotenda mambo maovu. Pande hizi mbili hutegemeana mno. Upande wa siasa hutegemea upande wa dini katika kukamilisha mambo yake na kadhalika baadhi ya masuala ya dini hutegemea maamuzi ya kisiasa katika kukamilisha malengo yake. Jirani mmoja wa Shaaban Robert aliyejitambulisha kwa jina la Mwanahamisi Mwinyimvua alitueleza kuwa:

> *Shaaban Robert ni mtu aliyekuwa amejaaliwa na Allah Subhana Wataala kipaji cha hali ya juu mno katika kuona mbali. Alijaaliwa kutambua kuwa hakuna jambo linaweza kufanikiwa katika maisha bila watu kuungana na kuwa pamoja katika kufikia utii wa sheria katika nchi. Aliamini kuwa siasa peke yake haiwezi na dini peke yake pia haiwezi isipokuwa kwa kushirikiana kwa pamoja. Alifika mahali akaelekeza kuwa hata dini moja peke yake haiwezi kuleta utawala wa sheria katika Ardhi na akapendekeza dini zote ziungane ziwe kitu*

> *kimoja. Nikitazama katika hali ya maisha ya leo ninaona moja kwa moja kuwa mawazo ya Shaaban Robert yaliona mbali mno. Hivi sasa watu wanazungumza juu ya dini na dini kuungana na kuheshimiana, vyama vya kisiasa kuungana na kuheshimiana na kwa ujumla kuheshimu sheria na mamlaka ya nchi. Hivyo, ninashauri serikali ihuishe ari ya kujisomea vitabu kwa wananchi wake na vitabu vya Shaaban Robert vichapishwe kwa wingi na visomwe na wananchi wote (Mwanahamisi Mwinyimvua, 16/08/2013).*

Maelezo haya ni ya kweli na ushahidi wake unapatikana katika kazi mbalimbali za Shaaban Robert kama *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. *Kusadikika*, *Kufikirika*, *Siku ya Watenzi Wote*, *Adili na Nduguze* na *Utu Bora Mkulima*. Nukuu hii inatoa rai kwa serikali kuhakikisha kuwa vitabu vya Shaaban Robert vinachapishwa kwa wingi na hata ikiwezekana vigawiwe bure kwa wananchi wote wajisomee. Rai hii tunakubaliana nayo na ni vema watunga sera wakaichukua na kuifanyia kazi. Vile vile, itakuwa ni jambo la busara kwa kila raia kujenga tabia ya kujisomea vitabu ili aweze kupata uhondo uliyopo katika kazi za Shaaban Robert. Uhondo atakaoupata ni ule ambao utamfunza umuhimu wa kuheshimu na kutii sheria za nchi na mamlaka zake. Msisitizo unaotolewa katika nukuu hapo juu kuhusu kusoma vitabu vya Shaaban Robert ni muhimu kwani katika utafiti tuliyofanya tumegundua kuwa wapo watu wengi wasiovijua vitabu vya Shaaban Robert. Jambo la kusikitisha ni kuwa, baadhi ya hao wasiovijua vitabu hivyo ni wanafunzi wa shule za sekondari wa kidato cha Tano na Sita. Hawa ndiyo tunaowategemea kuwa viongozi wa baadaye ambao watatakiwa kutii sheria na mamlaka za serikali. Kama hawataivishwa katika kusoma vitabu hasa vya Shaaban Robert isitegemewe kuwa watakuwa raia bora, watiifu wa sheria na mamlaka ya nchi.

Nukuu hapo juu inaonesha kuwa Shaaban Robert alikuwa ni mtu mzalendo kwa nchi yake ambapo aliwafunza wananchi na viongozi wao namna ya kuishi kwa kuheshimu

na kutii sheria za nchi. Mafundisho aliyoyatoa yanapatikana katika kazi zake zote alizopata kuziandika. Leo, serikali na watu wote katika jamii wanalalamika kuwa vijana na wengi wa watu wazima hawana uzalendo na nchi yao. Uzalendo unakosekana kwa sababu watu hawaishi kwa kutii na kuheshimu sheria za nchi. Kumetokea ujangili wa kuuwa Tembo na Faru kwa kasi ya juu inayohatarisha kutoweka kwa wanyama hao waliingizialo taifa fedha nyingi za kigeni. Yapo matukio mengi ya vitendo vya rushwa na ufisadi katika nchi unaolisababishia taifa hasara kubwa. Utii wa sheria ni kitu muhimu mno ambacho kitasaidia kupunguza maovu haya na kuwafanya wananchi wote kuwa waadilifu na wazalendo kwa nchi yao.

## 4.4 Kujifunza Mambo kutoka Jamii nyingine

Kujifunza ni kitu endelevu katika maisha ya mwanadamu tangu anapozaliwa mpaka anapofariki dunia. Kujifunza kuko kwa aina kadha wa kadha hutegemeana na mazingira na fursa ya mjifunzaji. Kwa mfano kuna kujifunza katika mazingira ya shule ambapo wanafunzi hufundishwa masomo mbalimbali na walimu wao. Katika kufundishwa masomo mbalimbali pia hujifunza mambo mengi kupitia walimu wao na wanafunzi wenzao hususani juu ya tabia na mwenendo wa maisha yao. Mwisho wa masomo hayo mtoto hupata ujuzi na maarifa ambao atautumia katika maisha yake ya kila siku. Vile vile, kuna kujifunza mambo kutokana na uzoefu katika maisha juu ya kazi, mahusiano, ushirikiano, vita, njaa, misiba, uongozi na mengine yanayohusiana na hayo. Kujifunza si kwa mtu mmoja na kwa manufaa yake yeye mwenyewe bali pia kuna kujifunza kwa ajili ya masilahi mapana ya taifa lote. Hapa ndipo pale serikali inapotuma ujumbe wake kwenda kujifunza kwa jamii nyingine na

kuuleta ujuzi huo hapa nchini. Kwa mfano, tumeshuhudia kuwepo kwa ziara za viongozi kama Rais, Mawaziri, Wabunge na viongozi wengine wa kisiasa katika nchi nyingine kwa lengo la kujifunza. Misafara ya ziara za viongozi hao huambatana na wataalamu wa kada tafautitafauti za maendeleo ya taifa sambamba na wafanyabiashara wakubwa. Lengo kuu la kuwapo kwa wataalamu na wafanyabiashara ni kujifunza mambo mbalimbali yanayohusiana na fani zao katika nchi walizokwenda na kuja kuyatumia hapa nchini kwa maendeleo ya taifa. Pamoja na misafara ya viongozi huwa pia kunakuwa na ujumbe maalumu ambao hutumwa katika nchi fulani au eneo fulani ndani ya nchi kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali yenye tija kwa jamii. Shaaban Robert alikwisha liona jambo hili kuwa lina umuhimu mkubwa hata kabla nchi za Afrika, ikiwamo Tanzania, hazijapata Uhuru. Amelisawiri jambo hili katika *Kusadikika* pale aliposema:

> *Kwa rai zilizotolewa na watu wa Ardhi, na kwa mvuto wa ufanisi wao, mjumbe wetu alikuwa na haki ya kuitaka Kusadikika kuiga mwendo wa Ardhi. Katika maendeleo ya wanadamu Ardhi imekwenda hatua nyingi sana mbele kuliko ilivyofanya Kusadikika. Karibu maisha ya malaika yatafikiwa na watu wa Ardhi kama bidii zao zitafululiza. Hawana mabawa lakini huruka hewani kama ndege kwa vyombo. Hawana mapezi lakini huzama baharini kama samaki kwa vyombo vile vile. Umbali wa safari umekunjwa barani, baharini na hewani. Vitabu vyote vimekusanya mambo mabaya kwa ushahidi mwingi, na yaliyo mema kwa uangalifu mkubwa. Ushahidi wa mambo mabaya huwahadharisha juu ya misiba, na ule wa mambo mema huwahimiza kwenda mbele. Kwa njia hii wamefaulu katika mambo mengi sana. Sasa Shetani ana wivu juu ya watu wa Ardhi kwa sababu hawashawishiki tena upesi kama ilivyokuwa zamani.*
>
> *Watu wenyewe walihitilafiana kwa rangi, lakini kwa akili zao za namna ya ajabu walipatana sana. Pia walihitilafiana na Wasadikika kwa Uzazi. Wanawake wetu huzaa mapacha lakini wao ni nadra sana kufanya hivyo (Uk. 46-47).*

Nukuu hii inaonesha kuwa nchi ya Ardhini ilikuwa imefikia maendeleo makubwa ambayo yalistahili kuigwa na Wasadikika. Wananchi wa Ardhini walifikia hatua ya

kuishi maisha bora yasiyo kifani kutokana na kufanya kazi kwa bidii na kuheshimu sheria na kanuni za nchi. Mjumbe anabainisha kuwa nchi ya Ardhi haikuwa na rasilimali za kutosha ikilinganishwa na ile ya Kusadikika lakini ilikuwa na maendeleo ya hali ya juu kabisa. Haya ni mafunzo tosha aliyoyapata mjumbe huyu na kuyaleta mbele ya wananchi wote kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Kumbe unaweza ukawa na rasilimali kidogo lakini ukapata maendeleo na ukawa na rasilimali nyingi lakini usiwe na maendeleo. Mbinu wanazotumia hawa wenye rasilimali kidogo kupata maendeleo ni zipi? Na hawa wenye rasilimali nyingi wanafanya makosa ya aina gani mpaka wanashindwa kupata maendeleo ni yapi? Maswali haya yanapozunguka akilini mwa mjumbe bila shaka anapata mafunzo ya kutosha ambayo yatasaidia kuimarisha maisha ya Wasadikika. Hii ni faida ya kwenda kujifunza kwa watu wengine kuhusu masuala ya maendeleo.

Funzo lingine alilolipata mjumbe kutoka katika nchi ya Ardhi lilikuwa ni kuishi pamoja bila kubaguana kwa misingi yoyote ile ya rangi, dini, kabila, jinsia, kiwango cha elimu na mengine yanayofanana na hayo. Tafauti hizi ni za kawaida katika maisha na zitaendelea kuwapo kila siku hivyo, zisiwe ni sababu za kubaguana na kutoheshimiana baina ya wanadamu wanaoishi mahali pamoja au hata katika nchi tafautitafauti. Watu wanaposhirikiana na kuwa kitu kimoja katika maisha hupata maendeleo kwa kasi ya ajabu na maendeleo watakayopata huwasaidia watu wote wa jamii husika. Mambo haya yanayosemwa na Shaaban Robert ni matukio ya kisiasa yaliyokuwa yakifanywa na serikali ya Kikoloni dhidi ya raia wa Tanganyika na nchi nyingine zilizokuwa zimetawaliwa na Wakoloni. Wakoloni waliwaona watawaliwa kuwa si watu waliostahili heshima na upendo baina yao. Ingawa wao watawaliwa

ndiyo waliokuwa wakifanya kazi katika mashamba ya watawala na kuwazalishia mali nyingi zilizowapatia utajiri lakini hawakupewa dhamani yoyote na watawala hao. Hali haikuwa hivyo katika nchi ya Ardhi kwani watu wote walipendana na kuheshimiana na hatimaye kusaidiana. Vile vile, suala la ubaguzi si la kipindi cha Ukoloni pekee kwani hata leo lipo katika jamii zetu. Watu hubaguana kwa misingi ya dini, ukabila, rangi na ujinsia na kusababisha kuuana kwa misingi ya tafauti hizo. Funzo alilokuja nalo mjumbe kutoka nchi za ughaibuni linatakiwa kuheshimiwa na kusimamiwa vizuri ili kujiletea maendeleo hususani kwa nchi changa kama Tanzania.

Jambo jingine ambalo mjumbe amejifunza ni kuwa katika nchi ya Ardhi watu husoma vitabu kwa nia ya kujifunza mambo mengi muhimu katika maendeleo. Vitabu wanavyosoma ni vile vilivyoandikwa na waandishi wa nchi yao. Anasema, "vitabu vyao vimekusanya mambo mabaya kwa ushahidi mwingi, na yaliyo mema kwa uangalifu mkubwa." Kauli hii inaonesha kuwa waandishi wa vitabu walizingatia mambo yote muhimu waliyotaka wananchi wote wayapate na kuyaweka katika maandishi. Baada ya kuyaweka katika vitabu kila mtu alijenga tabia ya kujisomea na kujifunza mambo hayo kwa kina kirefu. Shaaban Robert ameitumia kauli hii kuwataka waandhishi wa Tanzania kuandika kazi zao kwa kuzingatia utamaduni na mambo ya msingi kuhusu maisha ya jamii zao kama yalivyo. Hii itawafanya wasomaji kupata maarifa mapya watakayoyatumia katika harakati za kujiletea maendeleo. Hali haiko hivyo hivi leo. Baadhi ya waandishi wa vitabu huandika vitabu kwa kutumia lugha zisizoeleweka kwa urahisi kwa wasomaji jambo linalowafanya wasipate elimu iliyokusudiwa kwa usahihi. Jambo analolisema

Shaaban Robert ni la kisiasa kwa sababu maamuzi ya kwamba lugha ipi au mambo yapi yaandikwe katika vitabu huamuliwa na wanasiasa. Hivi leo, Kiswahili kimekwama kuwa lugha ya kufundishia ngazi zote za elimu kwa sababu ya utashi wa kisiasa haujaamua hivyo. Zainab Shemhoza ambaye ni jamaa wa Shaaban Robert huko Vibambani Tanga anasema:

> *Shaaban Robert alikuwa ni mtu mmoja aliyeipenda sana lugha ya Kiswahili. Ukitazama kazi zake alizoandika utaona matumizi ya Kiswahili sanifu ambacho ni kitamu kwa ulimi wa kukisema na liwazo kwa masikio ya msikilizaji. Mpaka kufikia leo hakuna mtunzi hata mmoja wa fasihi ya Kiswahili ambaye amemfikia Shaaban Robert kwa ubingwa wa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa namna alivyokipenda Kiswahili alitunga shairi la Titi la Mama Litamu ambalo maudhui yake yanahusu lugha ya Kiswahili (Zainab Shemahoza, 16/08/2013).*

Matumizi ya lugha ya Wazawa katika uandishi wa vitabu vilivyolengwa kusomwa na wazawa hao ni muhimu mno kwa maendeleo ya taifa lolote lile. Funzo hili limeletwa na mjumbe aliyekuwa ameagizwa kwenda kujifunza katika nchi nyingine na kulileta funzo hili kwa ajili ya utekelezaji. Wakati umefika hivi sasa kwa nchi kama Tanzania kutekeleza mambo muhimu kama haya yahusuyo lugha ili kuwaletea wananchi maendeleo.

Nchi kama vile China, Japan, Korea, Denmark, Norwey na nyinginezo zimepiga hatua kubwa ya maendeleo katika sekta mbalimbali kutokana na kutumia lugha zao katika elimu na mambo yote ya msingi yanayolihusu taifa lao. Kwa nini Tanzania isiige mfano huo? Zipo sababu nyingi zinazotolewa na wanaopinga kutumika kwa lugha ya Kisawahili na sababu kubwa ikiwa ni Kiingereza ni lugha ya Kimataifa na kuacha kutumia lugha hiyo kutalinyima taifa maendeleo. Swali la kujiuliza ni kuwa, hizo nchi zilizoacha kutumia Kiingereza kama lugha ya kutolea elimu hazikutambua

kuwa Kiingereza ni lugha ya Kimataifa? Bila shaka zilifahamu hilo lakini ziliona kuna umuhimu mkubwa wa kutumia lugha zao katika kutolea elimu. Hii inaonesha kuwa ni kawaida ya serikali ya Tanzania kutumia fedha zake nyingi kutuma wajumbe kwenda kujifunza katika nchi nyingine kisha mafunzo wanayoyaleta hukataliwa na kutupiliwa mbali. Katika *Kusadikika* anasema:

> *Nimeshitakiwa kuwa nataka ufalme na kupingana na sheria. Sitaki jambo hata moja katika mambo haya mawili. Sharafa ya sheria ni kubwa sana. Nimo katika zizi lake kama ng'ombe. Sina budi kuitii. Ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini kusaidiwa. Kwa kuchechemea wajumbe wetu wamerudi zizini kutoka safari ndefu lakini hawakusaidiwa" (Uk. 48).*

Maneno haya ya "Karama" yanaonesha namna viongozi wanavyopinga kutekeleza mafundisho yanayoletwa na wajumbe ambao walitumwa na serikali hiyohiyo kujifunza kutoka kwa watu wengine. Hali hii huchangia kuongeza umasikini katika jamii kwani fedha zilizotumika kugharamia safari ya wajumbe hao nchi za kigeni ni kubwa ambazo zingeweza kutumika katika maeneo mengine ya maendeleo. Sasa fedha zimepotea na mambo yaliyoletwa na mjumbe au wajumbe yamekataliwa. Mfano huu wa kukataa mafunzo yaletwayo na wajumbe yanaweza kulinganishwa na namna serikali inavyokuwa msitari wa mbele kukataa maoni ya wananchi wao kila mara na kutekeleza yale wanayoona kuwa yanawafaa wao viongozi kwa mtazamo wao. Hufikia mahali wananchi hawashirikishwi katika maamuzi yanayowahusu. Kitendo hiki hulinyima taifa fikra nzuri na thabiti za kuleta maendeleo kwa wananchi. Imetokea kila mara serikali inapowashirikisha wananchi katika mambo mbalimbali ya maendeleo hufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuliko ikifanya yenyewe bila ya kushirikisha wananchi. Mfano mzuri ni ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari kwa kila kata uliofanikiwa vizuri kutokana na kushirikisha wananchi.

## 4.5 Masuala ya Jinsia

Masuala ya jinsia yamechukua nafasi kubwa katika midahalo na mikutano ya jumuiya ya kimataifa. Jamii nyingi duniani zimekuwa zikimfanya mwanamke kuwa ni msaidizi wa mwanamme katika mambo mbalimbali bila ya kumshirikisha katika masuala muhimu ya maendeleo yanayomuhusu yeye mwanamke (Koda, 2000). Hali hii imetokana na mfumo dume ambao umeota mizizi katika jamii nyingi za Kiafrika. Mwanamke amefanywa kuwa ni kiumbe wa kufanya kazi za ndani kama kufua nguo, kulea watoto, kusafisha nyumba, kuosha vyombo, kupika chakula, kumuhudumia mume, kuwahudumia ndugu wa mume na watu wengine wote ambao wapo katika nyumba yake. Ngaiza (2002) anaeleza kuwa kazi ambazo hufanywa na mwanamke katika jamii ni mzigo mzito unaomkwamisha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Wanawake hukosa fursa ya kusoma na kupata elimu ambayo ingewasaidia kujiajiri na kuajiriwa kama ilivyo kwa wanamume. Mfalme wa Kufikirika aliona taabu wanayopata wanawake katika nchi yake na kufanyiza huruma kubwa juu yao. Anasema:

> *Alijua kuwa wanawake pengine huweza kufanya msaada mwema. Katika nchi yake wanawake wengi hukumbukwa kwa matendo yao bora waliyotenda. Alikuwa tayari kupokea msaada uliyoletwa kwa hiari na mwanamke lakini kulazimisha kutendewa msaada hakupenda. Aliona kazi na faraja zitendwazo na wanawake katika maisha zilitosha kuwa mzigo mzito juu yao. Kuongeza kitu chochote juu ya uzito wao kwake lilikuwa ni jambo la kuambaa nyayo elfu moja. Asubuhi alipokuwa yeye na waziri kauli ya huzuni ilimtoka (Uk. 01).*

Dondoo hili linaonesha kuwa mfalme wa Kufikirika alifahamu bayana mzigo mzito waliokuwa nao wanawake katika maisha. Mfalme alifahamu kuwa wanawake ndiyo walioachiwa watoto na kuwalea wao wenyewe baada ya waume zao kuwatoroka.

Hali hiyo iliwafanya kuwa na mzigo mzito ambao ulistahili kusamehewa mambo kadhaa na serikali. Kwa mfano, tunaona mfalme akifafanua kuwa yeye huwa hahitaji msaada wa lazima kutoka kwa wanawake kwa sababu anajua majukumu mazito waliyonayo wanawake. Hii ni sawa na kusema kuwa mfalme aliwasamehe wanawake kulipa kodi ila kwa hiyari walilipa wanawake walioweza kufanya hivyo. Shaaban Robert anayasema haya kwa kukebehi serikali za Kikoloni ambazo hazikuwa na huruma kwa mwanamke kwani zilimtumikisha katika mashamba ya kahawa, pamba, katani, chai na mengineyo bila ya huruma yoyote. Serikali hiyo haikujali kuwa mwanamke alikuwa na majukumu mazito ndani ya familia na hivyo apunguziwe mzigo wa kufanya kazi na asamehewe kulipa kodi. Kupitia maelezo ya Shaaban Robert serikali ya kikoloni ilitakiwa kubadilika mara moja na kuwathamini wanawake.

Serikali zilizoingia madarakani baada ya Ukoloni zilijitahidi kwa kiasi kumkomboa mwanamke kutokana na mzigo mzito aliokuwa nao. Serikali ya Tanganyika kwa mfano, ilianzisha Elimu ya Bure kwa Wote iliyojulikana kama Universal Primary Educalion (UPE) na kuwafanya wanawake kupata fursa ya kupata elimu bila kipingamizi chochote (Nyerere, 1967). Itakumbukwa kuwa serikali ya Kikoloni ilitoa elimu kwa ubaguzi ambapo Waafrika waliowengi hawakubahatika kupata elimu ikilinganishwa na Wazungu, Wahindi, Waarabu na watoto wa Machifu ndiyo waliyopewa kipaumbele cha kupatiwa elimu. Kwa kufanya elimu kuwa bure watu wote walipata fursa sawa ya kuendelea mbele kielimu. Sambamba na hilo pia huduma za elimu zilifanywa kuwa bure kwa wananchi wote. Sera hizi ni nzuri na zimeendelea kuwapo katika nchi ya Tanzania ingawa kwa namna tafauti kidogo.

Akina mama wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano hupatiwa huduma za afya bure katika hospitali na vituo vya afya. Hii ni njia sahihi ya kuwasaidia wanawake kwa sababu wengi wao hawana uwezo wa kifedha wa kumudu gharama za matibabu. Hata hivyo, upatikanaji wa huduma hizo za bure huwa ni mgumu mno na si wa uhakika na kwa kiasi kikubwa umesababisha hali ya vifo vingi vya akina mama wajawazito na watoto. Mwajuma Kheri ambaye aliwahi kuwa jirani wa Shaaban Robert huko Vibambani Tanga alitueleza kuwa:

> *Shaaban Robert alikuwa ni mtu mwenye huruma mmo juu ya wanawake na ndiyo maana aliamua kuwatetea sana katika kazi zake. Jambo la kuitaka serikali kuwaonea huruma wanawake na kuwapatia huduma za msingi bure ni kitu muhimu mno kwa sababu akina mama wengi ni wamama wa nyumbani wasio na kipato chochote. Pia baadhi yao hupewa mimba na kuzalishwa watoto kisha kutelekezwa na wanaume wao. Hata hivyo, huduma zinatolewa bure kwa akina mama na watoto ni bure kwa maneno tu lakini si kwa vitendo. Mwanamke asiyekuwa na fedha anaweza asihudumiwe na nesi hata akajifungua kwa taabu na aidha kupoteza maisha yake yeye binafsi au ya kichanga chake. Fedha za hongo na rushwa zinazotolewa kwa manesi ili kuwahudumia akina mama wajawazito zilitosha kabisa kulipia gharama za matibabu hayo katika zahanati na hospitali za binafsi. Mimi kama mwanamke ninaiomba serikali iendelee kutoa huduma za afya bure kwa wamama wajawazito na watoto lakini iboreshe namna ya kutoa huduma hizo kwa kuwawajibisha watovu wa nidhamu kazini* (Mwajuma Kheri, 15/08/2013).

Maelezo haya ni sahihi na hayana mushkeli hata kidogo. Vitendo vya rushwa vinavyojitokeza katika jamii vinakwamisha juhudi za serikali za kuona wanawake na wanajamii wote wanapata huduma bora na nzuri. Mateso anayopata mama wakati wa kujifungua ni makubwa kiasi cha kuhurumiwa na siyo kutakiwa kutoa rushwa ndiyo ahudumiwe. Sambamba na hilo, ipo haja ya kuimarisha huduma za afya zinazotolewa bure kwa mama wajawazito na watoto ziwe nzuri na siyo ilimradi tu kwa kuwa zinatolewa bure.

Si hivyo tu bali pia, serikali ya Tanzania inaonesha kuanza kusahau mizigo waliyonayo wanawake na kuwaongezea mzigo mwingine mkubwa zaidi. Kitendo cha serikali kupandisha kodi za bidhaa kama vile mafuta ya taa na petrol kinaonesha serikali kuwasahau wanawake. Unapopandisha kodi ya mafuta ya taa unamfanya mwanamke kulazimika kutumia nishati ya kuni peke yake katika kupika chakula. Hali ikiwa hivi mambo mawili hutokea. Kwanza mwanamke hushindwa kumudu gharama za mafuta ya taa na kuni huwa ndiyo mbadala wake kwa upande mmoja. Kwa upande wa pili serikali imepiga marufuku ukataji wa miti kwa ajili ya kuni kwa nia ya kuhifadhi mazingira. Katika hali kama hiyo mwanamke hujikuta katika hali mbaya ya kugagazika asijuwe afanye nini na hatimaye kupata matatizo ya kisaikolojia.

Kwa upande mwingine, kodi ya mafuta ya petrol inapopandishwa inakuwa ni pigo kubwa kwa jamii nzima lakini hasa kwa mwanamke. Huduma za maji, umeme, vyakula, matibabu na nyinginezo hupanda maradufu na kuwafanya wanawake kuwa katika hali mbaya zaidi ikilinganishwa na wanaume. Wanawake ndiyo huachwa na watoto wakati mwingine bila ya kuachiwa fedha za matumizi. Kwa hali hiyo huumiza kichwa akijaribu kutafuta mbinu mbalimbali zitakazowezesha kupatikana chakula cha watoto. Mbinu anazofanya hugonga mwamba kutokana na bei za vyakula kuwa bei juu kutokana na kodi. Hali hii inawataka wanaoandaa bajeti ya nchi kuwa makini kwa kutilia maanani masuala ya jinsia katika bajeti wanazoandaa. Kwa bahati mbaya wapo waandaa bajeti ambao wanafahamu vizuri masuala ya jinsia lakini huwa wanayafumbia macho. Kitendo hiki kinawaumiza wananchi na kupoteza dhima nzima ya serikali kuwasaidia wanawake na jamii kwa jumla.

Katika *Kusadikika* pia kunaelezwa masuala ya jinsia ambayo yanaonesha namna wanawake walivyo na bidii katika uzalishaji mali na kujituma kwa bidii ya hali ya juu. Imekuwa ni jambo la kawaida kuona mwanamke akiongoza katika kuizalishia familia yake tafauti na mwanamume. Baadhi ya wanaume hutumia muda mwingi katika kufanya shughuli ambazo haziingizii familia kipato. Hupoteza muda katika pombe, kucheza bao, mazungumzo na mijadala katika vijiwe. Hutoka nyumbani asubuhi na kurudi usiku huku baadhi yao wakiwa wamelewa chakari na mfukoni hakuna hata senti tano. Wanaume wa aina hii husababisha matatizo katika ndoa ambayo wakati mwingine husababisha ndoa kuvunjika na watoto kuteseka. Katika nchi ya Kusadikika wanawake hawajali wanafanyiwa nini na wanaume bali wao wanafanya nini kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa familia zao na nchi yao. Shaaban Robert anasema:

> *Wanawake wote katika nchi hiyo huzaa watoto pacha. Hii ni habari ya ajabu sana lakini haionekani kuwa imepata kugusa ndoto za wazee. Wasimulizi bado kusimulia, wala haijawashawishi wapima kuitia nchi hiyo katika ramani. Labda kukosekana kwa habari za nchi hiyo katika ndoto za wazee, katika masimulizi na katika ramani kutafanya udhuru wangu wa kuisimulia hadithi yake kukubalika (Uk. Vii).*

Nukuu hii inaonesha kuwa wanawake katika nchi ya kusadikika walikuwa wachapakazi wasio kifani. Anaposema wanawake wote walikuwa wanazaa watoto pacha, anatumia lugha ya taswira na picha kuonesha namna wanawake walivyokuwa na bidii katika uzalishaji mali. Katika hali ya kawaida, wanawake wengi huzaa mtoto mmojammoja huku wachache wakizaa watoto pacha. Lakini ajabu ya nchi ya Kusadikika, kila mwanamke huzaa watoto pacha. Maana yake ni kuwa, kila mwanamke ni mchapakazi na mzalishaji mkubwa wa mali kwa ajili ya familia yake na taifa kwa jumla. Ni ukweli uliowazi kuwa wanawake ndiyo wanaojishughulisha

na biashara ndogondogo, kilimo, ufugaji, ufinyanzi na kazi nyingine zenye kufanana na hizo na kutokana na shughuli hizi wanapata kipato cha kulisha familia chakula, kulipa karo za shule za watoto na kulipia gharama za matibabu za watoto hao. Pia kupitia kipato wanachopata hulipa kodi na tozo katika mamlaka za serikali na hivyo kuliingizia taifa fedha.

Katika nukuu hiyo, Shaaban Robert anaonesha kuwa mchango mkubwa unaofanywa na wanawake katika kuleta maendeleo kwa familia na taifa hauthaminiwi wala kusisitizwa kwamba wanawake waongeze juhudi katika kazi. "Kitendo cha kila mwanamke kuzaa watoto pacha, ni kikubwa na cha kustaajabisha mno, lakini hakuna aliyekuwa akishangaa tukio hilo katika jamii." Kauli hii inaonesha hali ya kutokuwa na shukurani kwa wanawake kwa mchango mkubwa wanaoutoa kwa maendeleo ya taifa. Kauli hii imejengwa kitaswira katika kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na wanawake katika maendeleo ya familia zao na taifa kwa jumla. Kwa hali hiyo, ni wajibu wa serikali kutazama kwa makini namna bora zaidi ya kutoa huduma stahiki za akina mama na watoto ili kuwafanya kuwa imara katika kulitumikia taifa.

### 4.6 Amani, Umoja na Mshikamano

Dunia huwa mahala salama na bora kwa maisha ya wanadamu kutokana na kuwapo kwa amani, umoja na mshikamano baina ya wanajamii (Mpangala, 2007). Kuwapo kwa mambo haya matatu huwafanya wananchi kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na kujipatia huduma za msingi katika maisha yao ya kila siku. Kwa mfano katika nchi ya Tanzania, amani imedumu kwa miaka mingi ikilinganishwa na nchi nyingine za ukanda huu na kuifanya nchi hii kujulikana ni kisiwa cha amani. Imeitwa kisiwa cha amani kwa sababu kila pande kuna machafuko ya hapa na pale

ambayo husababisha kutokuwapo kwa amani. Kukosekana kwa amani hufanya wananchi kuishi kwa hofu na mashaka ambayo huwafanya wasijishughulishe na shughuli yoyote ya kujiletea maendeleo. Rugumamu (2005) anaeleza kuwa amani ni kivutio cha uwekezaji wa ndani na wa kimataifa na kukosekana kwa amani na usalama katika nchi hudhoofisha uwekezaji. Kutokana na umuhimu wa amani, mshikamano na umoja katika nchi, jumuiya ya kimataifa imeyafanya mambo haya kuwa moja kati ya ajenda zake za vikao vyake. Shaaban Robert aliona umuhimu huo miaka mingi iliyopita na akasisitiza kuenziwa kwa mambo haya katika maandishi yake. Katika *Kusadikika* anasema:

> *Karibu watu wote huko walichukia uchokozi kama aibu kubwa, na waliviapiza vita kama laana ipitayo kasi kwa viumbe waliojaaliwa busara ya haki; moyo wa wema; ulimi wa nasaha; masikio ya kusikilizana; macho ya uongozi; pua ya kutambua harufu; ushirika wa amani; ajali moja, na Mungu mmoja. Hapana kabisa kitu hata kimoja katika hivi alichopewa mtu kwa ajili ya uharabu. Siasa kubwa huko ilikuwa ni kuwaunganisha watu wote katika urafiki. Juu ya urafiki huo amani ya ulimwengu imekusudiwa kujengwa.*
>
> *Neno "uadui na mengine mabaya kama yajulikanavyo, watu walikusudia kujaribu kuyatoa katika lugha na kuyafuta katika vitabu. Kwa amri ya serikali matangazo yalienezwa juu ya njia panda, barabara kuu, na kila mahali pa mikutano ya watu ili kuzuia matumizi ya maneno hayo. Imekwisha thibitishwa huko kuwa kama kwa vita mshindwa hupata hasara; na mshindi kadhalika huandamwa na kisasi cha milele. Hapana mtu yeyote apendaye hasara ya kushindwa wala kisasi cha ushindi katika maisha yake (Kur. 17-18).*

Nukuu hii inaonesha umuhimu wa amani na umoja katika jamii na kuitaka serikali kuwa msitari wa mbele kudumisha amani katika jamii. Serikali ndiye mdau mkuu katika kujenga na kudumisha amani katika jamii. Serikali ikitaka amani itakuwapo na isipotaka pia amani na umoja wa kitaifa hautakuwapo. Mtunzi wa *Kusadikika* alilitambua hilo ndiyo maana akapendekeza mbinu kadhaa za namna ya kujenga na

kudumisha amani katika jamii. Katika jamii iliyopo sasa hivi bado jukumu kubwa la kujenga na kudumisha amani lipo katika mikono ya serikali na wananchi wote. Kuwapo kwa matumizi ya nguvu za dola katika kuwadhibiti wapinzani wa serikali ni moja ya mambo yawezayo kuvuruga amani, umoja na mshikamano katika jamii. Amani ikivurugika ni kazi ngumu sana kuirejesha. Shaaban Robert analisema hili pale anapoonya kuwa "hakuna mtu mwema anayekubali kupata hasara katika vita wala kisasi cha vita katika maisha yake yote." Kauli hii imejaa falsafa nzito itoayo mafunzo muhimu juu ya kutunza na kulinda amani iliyopo katika jamii isije ikapotea. Imetokezea katika nchi kadhaa zilizoingia katika vita kushindwa kurejesha amani iliyokuwapo hapo awali. Shehe Sultani Kombo wa Tanga Mjini barabara ya 8 aliyekuwa rafiki wa karibu wa Shaaban Robert anaeleza kuwa:

> *Mapinduzi ya viongozi kwa njia ya machafuko na vita yaliyofanyika katika nchi za Libya na Misri yamefanya nchi hizo kukosa utulivu na amani ya kudumu. Wapo walioshinda vita na kutwaa madaraka ya nchi hizo. Pia wapo walioshindwa katika vita hivyo na kupata hasara ya kupoteza madaraka na mali zao. Kwa hivyo, hakuna mshindi wa kweli katika vita hiyo kwani visasi vimetawala kwa watu kuuwana kila siku. Vita na machafuko hayo yamewafanya wananchi kuishi maisha ya mashaka ndani ya nchi yao kwa kutegemea kuuwawa wakati wowote. Watanzania tunatakiwa tutazame mifano hii ili tujiepushe nayo kwa kuwa iliyowapata ni wanadamu kama sisi na kwamba inaweza kutupata wakati wowote kama hatutaheshimu utawala wa sheria (Shehe Sultani Kombo, 19/08/2013).*

Maelezo haya yanaumana na ya Shaaban Robert yaliyodondolewa katika *Kusadikika* hapo juu kuhusu amani na mshikamano katika jamii. Dhambi ya vita na machafuko ni mbaya sana na huitafuna jamii kwa kasi ya ajabu isababishayo mauaji kwa watu wasio na hatia. Nchi zilizotajwa na mtafitiwa hapo juu ni mfano mzuri wa nchi nyingine za Afrika, Asia na Ulaya zilizopo katika vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Tukirejelea maelezo ya Shaaban Robert katika dondoo hapo juu tunaona akitoa maelekezo juu ya kuchukua tahadhari katika kutunza amani na mshikamano katika jamii. Anaonesha umuhimu huo kwa kutumia maneno kama busara ya haki, moyo wa wema, ulimi wa nasaha, masikio ya kusikilizana, macho ya uongozi, pua ya kutambua harufu, ushirika wa amani, ajali moja na Mungu mmoja. Maneno haya yameteuliwa kwa ustadi wa hali ya juu kuonesha umuhimu wa kutunza amani katika jamii. Maneno haya yanaonesha kuwa watu katika jamii huweza kuhitilafiana katika jambo lakini mazungumzo ndiyo njia pekee ambayo itafanya mambo yaende sawa kwani kutokana na mazungumzo maridhiano hufikiwa. Tunao mfano mzuri wa kutolea ili kuthibitisha maneno ya Shaaban Robert. Mfano huo si mwingine bali ni ule wa mchakato wa katiba mpya katika nchi ya Tanzania. Awamu ya kwanza ya mijadala kuhusu katiba hiyo bungeni ilimalizika kwa mvutano mkali baina ya UKAWA na wajumbe wa bunge hilo watokao upande wa CCM. Mvutano huo ulisababisha UKAWA kutoka nje ya bunge na kutoendelea kuhudhuria vikao vilivyokuwa vimebaki mpaka hapo madai yao yatakaposikilizwa na kukubaliwa na upande wa pili. Hivyo, muongozo unaotolewa na Shaaban Robert juu ya kufikia makubaliano kwa mambo muhimu yahusuyo amani, umoja na mshikamano wa kitaifa ni muhimu kuzingatiwa ili kuepusha nchi kuingia katika machafuko.

Katika *Kufikirika* mtunzi anaeleza juu ya kuwapo watu maalumu wa kulinda amani na usalama wa nchi kwa nia ya kuhakikisha kuwa amani hiyo inadumu. Haiwezekani amani ikawepo daima kama hakutakuwa na watu maalumu waliokabidhiwa dhima hiyo kwa ajira yenye kulipwa mishahara na marupurupu stahiki. Mfalme wa nchi ya *Kufikirika* anasema:

> *Nina majeshi ya askari walioshujaa, waongozi hodari na raia wema na watii ambao hawalingani na taifa lolote jingine katika maisha yake yote. Jina lake litachorwa kwa majohari, wa watu hawa na pia nashukuru kuwa bwana juu ya vitu vya faraja visivyokwisha… (Uk. 03).*

Nukuu hii inaonesha kuwa jeshi ndilo ambalo limepatiwa jukumu la kuhakikisha amani ya nchi inakuwapo katika maisha ya wanajamii ya kila siku. Jeshi hilo limeundwa kwa vikosi vya kila aina ambavyo ni vitiifu kwa kiongozi wa nchi juu ya amri yoyote itakayotolewa juu yao. Sambamba na uwapo wa jeshi hilo pia kuna raia ambao ni watiifu kwa serikali hiyo. Hapa Shaaban Robert anaonesha umuhimu wa mashirikiano baina ya jeshi na wananchi katika kufanikisha kupatikana kwa amani ya dunia. Jeshi hata liwe kubwa kiasi gani haliwezi kuzidi idadi ya wananchi wote wa nchi husika. Hivyo, kila raia akitoa ushiriano kwa jeshi hakuna shaka kuwa jeshi litakuwa kubwa zaidi. Pia, wananchi ndiyo ambao wanawafahamu wahalifu na wavunjifu wa amani kwa sababu wanaishi nao. Wakitoa msaada kwa jeshi kwa kuwafichua wahalifu na waovu kazi ya jeshi itakuwa rahisi na kila siku amani, umoja na msikamano wa kitaifa utaimarika zaidi na zaidi. Maelezo yanayotolewa na Shaaban Robert katika *Kufikirika* juu ya mashirikiano baina ya jeshi na wananchi ndiyo yametawala katika majukwaa ya kisiasa na vikao baina ya polisi na wananchi. Katika miaka ya karibuni kumeanzishwa polisi jamii ambapo lengo kuu hasa ni kuimarisha ulinzi na usalama kwa mashirikiano baina ya polisi na wananchi.

## 4.7 Hitimishi

Katika sehemu hii ya kwanza ya sura ya nne ya tasinifu hii kumewasilishwa na kuchambuliwa data za utafiti zilizolenga kutimiza lengo mahususi la kwanza. Lengo hili likiongozwa na swali la kwanza la utafiti lililenga kubainisha masuala ya kisiasa

yanayozungumzwa na Shaaban Robert katika riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Masuala ya kisiasa yaliyowasilishwa katika sehemu hii ni uongozi katika jamii; uongozi mzuri, uongozi mbaya, utii wa sheria, kujifunza mambo kutoka jamii nyingine, masuala ya jinsia na amani, umoja na mshikamano. Masuala haya ya kisiasa ndiyo yaliyotawala majukwaa ya siasa katika nchi zote za Afrika na Tanzania ikiwamo. Taasisi za Kimataifa kama Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa zimeyafanya mambo haya kuwa ni kigezo muhimu cha nchi kupatiwa misaada ya maendeleo na mashirika hayo (Rugumamu, 2005). Nchi inayoshindwa kutimiza masharti ya kuimarisha mambo hayo hukosa msaada na taasisi hizo kubwa za maendeleo duniani. Nchi ya Tanzania inajitahidi kwa kiasi kikubwa kuimarisha mambo haya ili kukidhi vigezo na kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kufikia vigezo hivyo yapo. Hata hivyo, zipo changamoto ndogondogo ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili kuhakikisha kuwa, kunakuwa na utawala bora, amani, umoja na mshikamano, utii wa sheria kwa viongozi na wananchi na uzingativu wa misingi ya usawa na haki baina ya jinsia katika jamii unakuwapo. Sehemu inayofuatia inazungumzia juu ya mbinu za kisanaa zilizotumiwa na Shaaban Robert katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

## 4.8 Mbinu za Kisanaa katika *Kusadikika* na *Kufikirika*

Lengo mahususi la pili la utafiti huu linashughulikia uchunguzi wa mbinu za kisanaa zinazotumiwa katika uwasilishaji wa masuala ya kisiasa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Shaaban Robert ni bingwa wa matumizi ya mbinu anuai za kisanaa katika utunzi wake wa riwaya. Miongozi mwa mbinu hizo ni matumizi ya methali, tashibiha, kejeli, chuku misemo, mtindo wa kishairi, wahusika bapa na mandhari ya

kiuhalisia mazingaombwe. Uwasilishaji na uchambuzi wa data katika sehemu hii utaanza na mbinu ya matumizi ya methali katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*.

### 4.8.1 Matumizi ya Methali

Methali ni kipera katika utanzu wa fasihi simulizi ambao umekuwapo tangu mwanadamu alipoanza kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha. Hii ni sawa na kusema kuwa, methali ni utanzu mkongwe unaoendana sawa na historia ya kuwapo kwa mwanadamu hapa ulimwenguni. Ni kazi ngumu kuweka methali kando katika utunzi wowote wa kazi ya fasihi kwa sababu methali zimejaa hekima na busara na humuongoza mtunzi kuifanya kazi yake kuwa na dhamira murua kwa wasomaji wake. Njogu na Chimerah (1999) wanafasili methali kuwa ni usemi wenye pande mbili zinazotegemeana na kukamilishana. Upande wa kwanza huwa ni swali na upande wa pili huwa ni jibu la swali hilo. Pia methali huwa na mtindo wa kishairi wa vina na mizani. Shaaban Robert anatumia methali kama mbinu ya kuwasilisha dhamira za kisiasa katika *Kufikirika* na *Kusadikika*. Katika kufikirika kwa mfano anasema:

> *Wafikirika wana methali nyingine isemayo kuwa mwenye haya hazai. Mimi sina haya hiyo hii leo. Kwa hivi nimewaita mtusaidie kwa njia yoyote ambayo yafaa. Hazina zangu zi wazi. Tayari kufanya malipo hata senti ya mwisho katika sarafu zangu iishe. Kila mtu afanye msaada katika jambo hili atapata ijara ya kazi yake; na mtu ambaye atafaulu atapata ijara mara mbili au zaidi kuliko wengine wote katika hazina za Kufikirika; zawadi na posho maridhawa katika maisha yake yote… (Uk. 06).*

Methali hii (*mwenye haya hazai*) inaonesha kuwa kiongozi wa nchi anaweza kupata tatizo na wananchi wake ndiyo watakaoweza kutatua tatizo lake. Mfalme anaonesha kuwa, kupata mamlaka na kuwa kiongozi huwezi kupatwa na shida ambayo itahitaji

msaada kutoka kwa wananchi wako. Anasema kwa kutumia methali kuwa, mwenye haya hazai methali ifananayo na ile isemayo mficha uchi hazai. Kwa hiyo akaona kuna haja ya kuondoa haya na kueleza tatizo lake kwa wananchi na bila ajizi walijitokeza watu wengi kumsaidia mfalme wao kupata mtoto. Matumizi ya methali hii yanatoa fundisho kuwa matatizo ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi ambayo yanaikabili nchi huweza kutatuliwa na wananchi wenyewe bila ya kutegemea msaada kutoka nchi nyingine. Hata hivyo, ni lazima viongozi wa serikali na hususani kiongozi mkuu wa nchi aone haja na akubali kuwashirikisha wananchi wake katika kutatua matatizo yanayowakabili.

Katika *Kusadikika* pia, mtunzi anatumia methali kuwasilisha masuala ya kisiasa kwa hadhira iliyokusudiwa. Anasema:

> *Kwa umbo la nje, mshitakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu, lakini kwa wasifu wa ndani, alikuwa na ajabu tatu. Kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima, kifuani alikuwa na moyo wa ushujaa, na kinywani ulimi wa ufasaha. Vipawa hivi vilikuwa katika siri kubwa sana. Hata baadhi ya wasiri wake hawakuweza kusikia kuwa alikuwa na hazina kama hizi. Alikuwa na tabia ya kuficha siri kama kaburi lifunikavyo maiti. Alijizoeza kuvitumia vipawa mpaka vilikuwa tayari kutumika siku yoyote katika maisha yake (UK. 08).*

Katika nukuu hii kuna matumizi ya methali, "siri ya maiti aijuaye kaburi." Kwa muktadha wa masuala ya kisiasa yanayotafitiwa katika tasinifu hii methali hii ina maana kubwa mno kwa wananchi wote. Kwanza kabisa ni umuhimu wa kuficha siri za nchi yao kwa watu wengine ambao wanaweza kuwa maadui. Si kila kitu kiwe kibaya au kizuri kinafaa kusemwa mbele za watu kwani huweza kuwa ni silaha itakayotumiwa na adui wako kukuangamiza. Tumesema jambo zuri au baya tukiwa na maana pana, kwa mfano, yawezekana katika nchi kuna rasilimali nyingi ambazo

hazijatumika kutokana na nchi kukosa utaalamu wa uwezo wa kufanya hivyo. Jambo zuri la kufanya hapa ni kutunza siri wakati mipango ya kutafuta ujuzi na uwezo ikifanyika. Baada ya ujuzi kupatikana hakuna tatizo lolote kutoa siri hiyo kwa watu wengine kwa sababu ujuzi upo na hakuna awezaye kuiba rasilimali hiyo. Katika nchi ya Tanzania kumegundulika rasilimali za aina mbalimbali wakati ambapo nchi haina uwezo wa fedha, utaalamu na teknolojia ya kunufaika na rasilimali hizo. Viongozi wa serikali wakaamua kushirikisha wawekezaji kutoka nchi zilizoendelea kwa nia ya kuja kuwekeza hapa nchini. Kwa bahati mbaya uwekezaji uliofanywa ulikuwa ni wa kuneemesha upande wa wawekezaji zaidi kuliko serikali. Hii ilisababishwa na kutoa siri kabla ya kujiandaa vizuri kukabiliana na matokeo ya siri hiyo kufahamika kwa wawekezaji. Mwanaidi Kimweri ambaye aliwahi kuwa rafiki na mke wa Shaaban Robert wa barabara ya 2 Tanga Mjini alitueleza kuwa:

> *Mimi ninavutiwa mno na riwaya za Kusadikika na Kufikirika kwa sababu riwaya hizi zina matumizi ya methali nzuri zenye kuvutia. Unapokutana na methali fulani unaona moja kwa moja inavyowiana na kile kinachosemwa na Shaaban Robert. Methali hizo zinasaidia kutupatia sisi wasomaji urahisi wa kupata dhamira katika riwaya hizi mbili zilizoandikwa kimiujizaujiza (Mwanaidi Kimweri, 14/08/2013).*

Maelezo haya ni ushahidi tosha kuwa Shaaban Robert ni bingwa katika matumizi ya methali ambazo hurahisisha uelewekaji wa dhamira kwa wasomaji wa riwaya zake zilizoandikwa katika mandhari ya hewani yaani nchi zinazoelea. Msomaji akikutana na methali anapata uhalisia kuwa kile kinachosemwa kutokea katika nchi ya Kusadikika au Kufikirika kinatokea pia katika nchi za kawaida alizozizoea.

### 4.8.2 Matumizi ya Tashibiha

Tamathali ya usemi itumikayo kufananisha vitu viwili kwa kutumia maneno ya ulinganisho hujulikana kama tashibiha na wakati mwingine tashibihi (Wamitila,

2008). Maneno ya mlinganisho yanayotumiwa na tamathali hii ni “kama,” “sawasawa,” “mithili ya,” “na sawa na.” Matumizi ya maneno haya hufanya vitu viwili ambavyo kimsingi havifanani kwa sifa na umbo kufanana na kuonekana kuwa ni sawasawa. Tashibiha hutumika kwa ajili ya kutoa msisitizo kwa msomaji hasa kwa kumfanya apate uhalisia wa jambo hata kama kinachoelezwa ni cha kiuhalisia ajabu au uhalisia mazingaombwe (Khamis, 2007). Riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* zimeandikwa kwa kuzingatia mkondo wa kiuhalisia mazingaombwe na kutumika kwa tashibiha huzifanya kazi hizi kumwelekeza msomaji katika uhalisia. Katika *Kusadikika* mtunzi anatumia tashibiha kufafanua na kusherehesha dhamira za kisiasa kwa wasomaji wake. Kwa mfano:

> *Watu wenyewe walihitilafiana kwa rangi, lakini kwa akili zao za namna ya ajabu walipatana sana. Pia walihitilafiana na Wasadikika kwa Uzazi. Wanawake wetu huzaa mapacha lakini wao ni nadra sana kufanya hivyo. Maisha ya watoto wetu wengi hayana salama kuliko maisha ya watoto wao kidogo yalivyokuwa. Watu hao walisema lafudhi mbalimbali zilizoonesha matokeo ya mchafuko wa lugha usemwao kuwa ulitokea zamani katika Ardhi. Lakini jitihada zote zilikuwa zikifanyizwa ili waweze kusikilizana kama watu wenye lugha moja tu. Yamkini hilo litawezekana kwa sababu watu wa huko* ***wana bidii inayowaka kama moto*** *(Uk. 46-47).*

Nukuu hii inaeleza jitihada zinazofanywa katika nchi ya Ardhi ili kuwafanya wananchi wake wazungumze lugha moja tu. Mtunzi anaonesha kuwa watu wa nchi hiyo huzungumza lugha tafautitafauti lakini haikuwa sababu ya wao kuhitilafiana katika mambo ya msingi yanayohusu nchi yao. Hata hivyo ilionekana kuwa ipo haja ya watu hao kuwasiliana kwa lugha moja tu. Jambo hili kwa hakika ni gumu kwa kuwa si kazi rahisi mtu kuacha lugha yake ya asili na kuzungumza lugha moja tu itakayokuwa imeteuliwa. Mtunzi anatumia tashibiha, *wana bidii inayowaka kama moto*, kwa hiyo matumizi ya lugha moja tu yatawezekana. Bidii ya kufanya jambo na

moto ni vitu tafauti kabisa lakini kwa ilivyotumika hapa inaonesha kuwa jitihada zinazofanywa ili kutumia lugha moja ni kubwa mno na zitafanikiwa.

Tashibiha "wana bidii inayowaka kama moto" imetumika pia kuonesha kuwa katika nchi hiyo wananchi wakiamua kufanya jambo lao lazima likamilike. Jambo hilo linaweza kuwa ni kilimo, elimu, afya, kuimarisha uongozi, ufugaji, ujengaji wa barabara, uchimbaji wa visima vya maji safi na uhifadhi wa mazingira. Kwa kuwa wana bidii inayowaka kama moto basi inakuwa ni kazi rahisi kwao kutekeleza kila jambo walilodhamiria kutekeleza.

Matumizi ya tashibiha yanajitokeza pia katika *Kufikirika* kwa nia ile ile ya kuwasilisha dhamira kwa hadhira ya kazi hii. Mtunzi anasema:

> *Kazi kubwa katika nchi hiyo ni ukulima, ufugaji, uhunzi, useremala, uashi, uganga, uaskari, ubaharia, ualimu, uandishi, biashara, dini, ufumaji na ushonaji. Chini ya kazi hizi zilifuata nyingine zote ambazo huleta ustawi katika taifa. Mkulima alitakiwa awe stadi na mwelewa wa kila njia ya ukulima wa nyakati mbalimbali za kazi hiyo.* ***Shamba la mtu mmoja lilikuwa kubwa kama jimbo*** *(Kur. 15-16).*

Matumizi ya tashibiha, **shamba la mtu mmoja lilikuwa kubwa kama jimbo** inatoa msisitizo kuwa wakulima wa nchi ya Ardhi walikuwa wachapakazi mno na nchi ya Kufikirika ilipaswa kuiga mfano huo ili kujiletea maendeleo. Kwa kilimo cha aina hii ilikuwa si rahisi nchi ya Ardhi kupatwa na njaa. Sambamba na hilo, tashibiha hii imetumika kama kejeli kwa serikali ya Kikoloni ambayo ilichukua mashamba makubwa na kuwaacha wananchi bila hata kipande kidogo kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula. Mashamba waliyochukuwa Wakoloni yalitumika kulima mazao ya biashara kama pamba, kahawa, katani, na chai. Kwa hiyo ili nchi ya Kufikirika

iweze kuendelea ilihitaji kuwapatia wakulima wake ardhi ya kutosha kuendeleza kilimo.

Yanayosemwa katika tamathali ya usemi hapo juu yanajitokeza katika hali halisi ya maisha ya jamii ya leo. Kumekuwapo malalamiko kuwa wapo baadhi ya wawekezaji ambao wamemilikishwa mashamba makubwa na serikali na kuyatelekeza huku wananchi wa kawaida wakikosa ardhi ya kulima. Malalamiko haya yamefika mpaka katika ofisi ya Waziri Mkuu na kuagiza kila mkoa kupeleka orodha ya mashamba hayo katika ofisi yake ili aweze kumshauri Rais kubadilisha umiliki.

### 4.8.3 Matumizi ya Kejeli

Mbinu nyingine ya kisanaa inayotumiwa na Shaaban Robert katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika *Kusadikika* na *Kufikirika* ni kejeli. Kejeli ni mbinu ya kueleza jambo kinyume na lilivyo katika uhalisia. Kwa mfano mtu anaweza kusifiwa kuwa yeye ni kiongozi mwadilifu sana katika jamii lakini kumbe si kweli ni mla rushwa na fisadi wa kutupa (Njogu na Chimerah, 1999). Katika *Kufikirika* kuna matumizi ya kejeli dhidi ya utawala wa Kikoloni na penngine utawala uliopo hivi sasa. Mtunzi anasema:

> *Serikali ya Kufikirika ililazimisha sana ustadi wa watu wake katika kazi zote. Kwa hivi Wafikirika waliidilika katika njia nyingi sana. Nchi ilikuwa ina serikali imara, waongozi wa ubongo mzuri, mahakimu wa haki, waandishi bora, wanachuoni mufti, wasafiri na wagunduzi wavumilivu na wajasiri, mabaharia wa moyo mkuu na wenye kuthubutu na askari wa miili migumu, mishipa minene, kano kavu zenye nguvu na shabaha nzuri… (Uk. 17).*

Nukuu hii inatumia kejeli pale inapodai kuwa serikali ya Kufikirika ililazimisha wananchi wake kuwa na ujuzi kwa kila fani. Hii ni kejeli kwa serikali ya Kikoloni ambayo ilitoa elimu kwa ubaguzi na kuwanyima Waafrika wengi kupata fursa ya

kusoma katika shule zilizoanzishwa na serikali hiyo. Kuandikwa kwa kitabu hiki katika kipindi cha ukoloni na serikali ya kikoloni ilikuwa haifanyi haya yasemwayo ni kejeli kwa serikali hiyo. Pia anasema kuwa serikali hiyo ilikuwa na viongozi wenye ubongo mzuri. Hii nayo ni kejeli kwa utawala wa Kikoloni kwa sababu kama viongozi hao wangekuwa na ubongo mzuri basi wangewajali wananchi wa Tanganyika na Afrika kwa jumla kwa sababu ndio waliozalisha mali.

Kwa upande wa serikali iliyopo hivi sasa hii pia inaweza kuwa ni kejeli hasa pale inaposisitiza wananchi wake kupata elimu za fani mbalimbali lakini baadaye haiwatumii wataalamu hao katika kazi mbalimbali. Imetokea katika baadhi ya sekta serikali kutoa kandarasi kwa makampuni ya ujenzi kutoka nje ya nchi hali ya kuwa kuna wataalamu wa ndani amb``ao wanaweza kufanya kazi hizo. Malalamiko mengi yametokezea katika kandarasi za ujenzi wa nyumba na barabara ambapo kipaumbele hutolewa kwa makandarasi wa kigeni kuliko wazawa. Pamoja na lawama hizo lakini bado kuna ukweli kuwa makandarasi wa ndani hawajawa na mtaji, vifaa na teknolojia ya hali ya juu waliyonayo wale wa kigeni. Hivyo, ni wajibu wa kandarasi za ndani kujiimarisha katika maeneo hayo ili kuweza kushindana na wageni katika kandarasi za hapa nchini na hata kimataifa.

Matumizi ya kejeli yanatumika pia katika *Kusadikika* kwa namna kama ile ile ambayo inaonekana katika *Kufikirika*. Mtunzi anasema:

> *Kwa sababu ya kudumisha sheria, dini, na mamlaka; na kwa wajibu wa kazi yangu, lazima nidhihirishe mbele ya baraza hii kuwa si jambo jema hata kidogo kuamuru madarasa ya utaalamu uwezao kuwa daraja, ambayo chini yake utapita mkondo mkubwa sana wa mambo ya kuichafua salama ya Kusadikika kwa dharau, ukaidi na jinai. Matendo ya mshitakiwa lazima yakomeshwe kwa adhabu ya mwisho katika sheria. Kazi kubwa na yenye thamani adhimu*

> *ilitendwa katika kuzitengeneza na kuzidumisha sheria hizi. Haivumiliki kuziona zinavunjika kwa matendo ya mtu mmoja anayetafuta ubarakala, asiyeaminika, mchache wa shukurani na mjeuri. Nguvu ya sheria za nchi lazima ithibitishwe juu yake ili mtu mwingine yeyote asithubutu kuzidharau (Kur. 05-06).*

Nukuu hii inaonesha kejeli kwa serikali ya Kikoloni kwa kitendo chake cha kuzuia watu wasijifunze mambo ambayo yana masilahi kwa taifa lao. Serikali ambayo inasisitiza utawala wa sheria na kumtaka kila mwananchi atii sheria za nchi leo unakataza watu kujifunza sheria. Hii inaonesha kuwa lipo jambo ambalo walikuwa wanaficha na hawakutaka wananchi walijue kuhusu sheria hizo ili waendelee kuwadhulumu na kuwanyanyasa. Kimsingi, serikali ya kikoloni iliwakataza kufanyika kwa mambo ambayo walidhani kuwa yatahatarisha uwapo wa serikali yao. Kwa mfano, walikataza uandishi wa kazi za fasihi ambazo zilionesha kutokukubaliana na metendo ya serikali hiyo. Iqbali, mtoto wa Shaaban Robert alitueleza kuwa:

> *Baba yangu alipata kunisimulia kisa cha kuamua kuandika kazi zake kwa mtindo wa kiajabuajabu. Alisema kuwa katika kipindi cha utawala wa serikali ya Kikoloni ya Kijerumani alipata kuandika riwaya ya Maisha Yangu. Mambo aliyoyaeleza humo yalikuwa yanakosoa utawala huo kwa lugha ya wazi. Ndipo watawala hao walipomwingiza katika daftari la watu hatari na kutaka kumuua. Kwa bahati Ujerumani ilinyang'anywa makoloni yake na kupatiwa Waingereza, Wafaransa na mataifa mengine ya Ulaya. Tanganyika ilikuwa ni moja kati ya makoloni yaliyowekwa chini ya utawala wa Waingereza na hivyo kusalimika kuuwawa kwa Shaaban Robert. Kwa hiyo, akaona ni vema aandike kazi zake zilizofuatia kwa mtindo wa Kusadikika na Kufikirika ili serikali ya Kiingereza nayo isije ikakusudia kumuua.*

Maelezo haya yanaonesha kuwa serikali ya kikoloni ilikuwa haiko tayari kuona inakosolewa kwa jambo lolote ambalo inalifanya kinyume na matakwa ya wananchi. Hivyo, walifanya kila njia kuhakikisha kuwa wanazuia ukosolewaji wa aina yoyote

ile dhidi yao. Ilikuwa si kazi rahisi kwa serikali ya Kikoloni kumtuhumu Shaaban Robert kuwa aliikosoa serikali ya Kikoloni kwa sababu nchi aliyoielezea ilikuwa si ya kiuhalisia.

### 4.8.4 Matumizi ya Mandhari

Mandhari ni mahali ambapo kazi ya fasihi inatukia na kufanyikia (Wamilita, 2002). Mandhari inaweza kuwa halisia au ya kubuni (Kezilahabi, 2003). Mandhari halisia ni ile inayohusisha miji, vijiji, makazi ya wananchi ambayo yapo na yanaonekana na kufahamika kwa watu. Mandhari ya kubuni huwa haina uhalisia unaofahamika kwa wasomaji lakini inaeleza mambo ambayo yanatokea katika ulimwengu halisi. Shaaban Robert ni miongoni mwa watunzi wa riwaya atungaye riwaya zake kwa mandhari ya kubuni ijulikanayo kama uhalisiaajabu au uhalisia mazingaombwe (Khamis, 2007). Matumizi ya mandhari ya aina hii yanajitokeza katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Kwa mfano katika *Kusadikika*, mandhari yake ni hii:

> *Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake hufikirika kwa mawazo tu. Nchi hiyo iko katikati ya mipaka sita. Kwa upande wa Kaskazini imepakana na upepo wa Kaskazi, na kwa upande wa Kusini imepakana na upepo wa Kusi. Mashariki imepakana na Matlai, na Magharibi mpaka wake ni upepo wa umande. Kwa kuwa nchi yenyewe inaelea katika hewa kama wingu, zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mingine miwili. Mipaka miwili yenyewe ni hii. Kwa juu nchi hiyo imepakana na Mbingu, na kwa chini imepakana na Ardhi (Kur. Vii).*

Nukuu hii inathibitisha kuwa nchi ya Kusadikika si nchi inayofahamika katika uhalisia kwani ipo angani na inaelea kama wingu. Pamoja na kuwa nchi hii ipo angani lakini inaeleza mambo yanayotokea katika ulimwengu halisia. Mambo yanayoelezwa ni uongozi mbaya na mzuri katika jamii, masuala ya jinsia, utii wa sheria, kujifunza kutoka kwa wengine na amani, umoja na mshikamano. Mambo

haya ni halisia, yapo katika nchi kama Tanzania, Kenya, Uganda, Marekani, Uingereza, China, Australia na nchi nyingine duniani. Shaaban Robert aliamua kutumia mandhari ya aina hii kutokana na sababu zilizotolewa na mwanawe tulizozidondoa hapo juu.

Katika *Kufikirika* pia ametumia mandhari ya aina hiyo hiyo ya kiuhalisiaajabu au uhalisiamazingaombwe. Kwa mfano:

> *Kufikirika ni nchi moja kubwa kati ya nchi za dunia. Kaskazini imepakana na nchi ya Anasa. Kusini nchi ya Majaribu, Mashariki bahari ya kufaulu na Magharibi safu ya milima ya Jitihadi. Ramani ya nchi hiyo ni adimu kupatikana kwa sababu nchi yenyewe haiandikiki ila kufikirika kwa mawazo tu. Njia ya kwenda nchi hiyo hukanyangwa kwa fikra siyo nyayo. Wafikirika ni wengi nao ni wazazi mno. Nyumba moja kuwa ina watoto wanane hata kumi na sita si jambo la ajabu. Jumla ya Wafikirika karibu sawa na nusu moja ya watu wa makabila yote mengine yaliyomo duniani… (Uk. Vii).*

Hapa napo tunaoneshwa kuwa nchi ya Kufikirika ipo mawazoni tu mwa watu haiandikiki wala haionekani. Ukitaka kufika katika nchi hiyo, unatakiwa kutumia njia ya fikira na siyo kutumia nyayo za miguu. Hii ni si nchi ya kawaida tunayoifahamu ni nchi ya ajabu mno. Kwa kutumia mandhari ya aina hii Shaaban Robert amefaulu kusawiri madhila mengi yaliyofanywa na serikali ya Kikoloni kwa wananchi wa nchi za Afrika na kwingineko kulikotawaliwa na Wakoloni hao. Aliyoyasawiri ni uporaji wa mali za wananchi, utawala wa mabavu, dhuluma ya haki, elimu duni kwa wananchi, huduma duni za afya kwa wananchi na kulazimisha wananchi kufanya kazi katika mashamba ya Wakoloni kwa malipo kidogo. Kwa kutumia mandhari halisia asingeweza kusawiri mambo yote haya na kazi zake zikaruhusiwa kuchapwa na kusomwa na wananchi mbele ya serikali ya Kikoloni.

### 4.8.5 Matumizi ya Wahusika Bapa

Shaaban Robert anatumia wahusika aina ya bapa katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira yake. Wahusika ni wale ambao wanatumiwa na mtunzi wa kazi za fasihi kubeba maudhui ambayo mtunzi anataka hadhira yake iyapate (Mlacha na Madumulla, 1991). Kuna wahusika wanadamu, wanyama, wadudu, mizimu, miti, mawe na mashetani (Njogu na Chimerah, 1999). Shaaban Robert hutumia zaidi wahusika wanadamu kuliko wa aina nyingine. Katika wahusika wanadamu anaotumia hupendelea zaidi kutumia wahusika bapa. Wahusika hawa ni wale ambao huwa na tabia fulani ambayo haibadiliki tangu mwanzo wa hadithi mpaka inamalizika. Mlacha na Madumula (1991) wanaeleza kuwa mhusika bapa huwa haonekani kukuwa kitabia, kimatendo na kisaikolojia. Huonekana kuwa na msimamo mmoja tangu mwanzo wa hadithi mpaka mwisho bila ya mabadiliko yoyote.

Shaaban Robert anatumia wahusika wa aina hii kwa dhima maalumu ya kutaka wanajamii kuiga mwenendo mwema na kuacha mwenendo mbovu uoneshwao na wahusika. Katika *Kusadikika* kuna wahusika wawili wenye sifa za ubapa. Wahusika hao ni Karama na Majivuno. Karama ni mtu anayesawiriwa kuwa ni mtu mwema tu tangu mwanzo wa hadithi mpaka mwisho wa hadithi hiyo. Majivuno ni mhusika anayesawiriwa kama mtu mwenye majivuno na dharau kwa watu wengine tangu mwanzo mpaka mwisho wa hadithi ya *Kusadikika*. Kwa mfano katika *Kusadikika* anasema:

> *Waziri wa Kusadikika alikuwa mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi. Kwa hivi aliitwa Majivuno… Umri wake mkubwa ulizifanya nywele zake kichwani kuwa nyeupe kama fedha. Kwa haiba hii aliweza kuyavuta macho ya watu; na kwa ufasaha wa maneno aliweza kufanyiza fungu au mwamba wa kuyavunja maisha ya mtu yeyote kama chombo. Kipawa chochote cha mtu kama*

> *hakikuongozwa vema huweza kuwa hatari au maangamizi kwa wengine. Mtu huyu alikuwa maarufu na mashuhuri lakini alijaa tadi na inda kama hadithi hii inavyosimulia (Uk. 01).*

Nukuu hii inampamba Majivuno, waziri katika serikali ya Kusadikika aliyeshika madaraka kwa miaka mingi na hakuwahi kubadilika kitabia. Majivuno aliyokuwa nayo yalidumu katika vipindi vyote vya utawala wake. Mtu yeyote aliyeonekana kupingana na serikali ya Kusadikika alishughulikiwa kwa adhabu kubwa kwa maelekezo ya waziri Majivuno. Kwa ukali na ukatili aliokuwa nao hakuna aliyeweza kunusirika kuadhibiwa vikali na hata kuuwawa kama ilibidi. Nukuu inaonesha kuwa majivuno aliweza kufanya kila linalowezekana kuhakikisha alichokitaka yeye kinafanikiwa hata kama si sahihi wala haki kufanya hivyo. Sambamba na hilo, alikuwa ni mtu aliyenata, kujisikia na dharau kubwa kwa wananchi hohehahe. Hizi ni tabia za uhusika bapa kwa sababu hazikubadilika tangu alipoanza uwaziri akiwa kijana ndogo mpaka sasa ana mvi nyeupe kama fedha.

Majivuno ni mhusika anayewasilisha sura kamili ya viongozi waliokuwa katika serikali ya Kikoloni ambao walikuwa katili kwa raia. Viongozi hao hawakuwa na huruma kwa mwanadamu yeyote aliyeonekana kukinzana na mamlaka ya Kikoloni. Shaaban Robert amemtumia mhusika huyu kuonesha kuwa hafai kuwa kiongozi mwema na hivyo serikali huru za Afrika zisiige mfano wake. Katika riwaya yote ya *Kusadikika*, hakuna hata mahali pamoja ambapo tunaoneshwa kuwa Majivuno alipata kutenda wema. Katika hali ya kawaida ya mwanadamu haiwezekani majivuno asitende wema hata kidogo kwa familia yake na watu wanaomzunguka. Shaaban Robert alilifahamu hilo lakini akaamua kumsawiri Majivuno katika hali hiyo ili kuisawiri barabara dhamira ya uongozi mbaya hasa ule wa Kikoloni kwa Waafrika.

Kwa upande mwingine tunakutana na mhusika Karama ambaye anasifika kwa sifa nzurinzuri tangu mwanzo wa riwaya mpaka mwisho. Sifa zake ni tafauti kabisa na zile za Majivuno. Mtunzi anasema:

> Kwa umbo la nje, mshitakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu, lakini kwa wasifu wa ndani, alikuwa na ajabu tatu. Kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima, kifuani alikuwa na moyo wa ushujaa, na kinywani ulimi wa ufasaha. Vipawa hivi vilikuwa katika siri kubwa sana. Hata baadhi ya wasiri wake hawakuweza kusikia kuwa alikuwa na hazina kama hizi. Alikuwa na tabia ya kuficha siri kama kaburi lifunikavyo maiti. Alijizoeza kuvitumia vipawa mpaka vilikuwa tayari kutumika siku yoyote katika maisha yake (UK. 08).

Nukuu hii inaonesha kuwa Karama ni mtu aliyekuwa mwema kupita kifani. Aliweza kuficha siri isifahamike kwa mtu yeyote hata wale ambao ni wasiri wake. Kimsingi hili jambo jema mno mtu kuweza kuficha siri hata kwa watu wa karibu kwani si kila kitu hufaa kuzungumzwa mbele za watu. Hata hivyo, katika hali ya ubinadamu upo uwezekano Karama alikwishawahi kuteleza na kutoa siri ambayo au ambazo hakutakiwa kuzitoa kwa mtu au watu wengine. Ubinadamu ndivyo ulivyo. Shaaban Robert alilifahamu vizuri suala hili lakini akaamua kufanya hivyo, ili kuonesha umma umuhimu wa kuwa watu wema wasio na majivuno katika jamii.

## 4.9 Hitimishi

Dhumuni mahususi la pili limetimizwa kutokana na maelezo yaliyotolewa katika sehemu hii. Shaaban Robert ni bingwa wa matumizi ya mbinu mbalimbali za kisanaa katika kuwasilisha masuala ya kisiasa kwa hadhira yake. Hata hivyo, kwa nia ya kutimiza dhumuni mahususi la pili la utafiti huu tumezungumzia mbinu tano tu. Mbinu hizo ni matumizi ya methali, tashibiha, kejeli, mandhari na wahusika. Mbinu hizi kwa pamoja zimewezesha uelewekaji wa masuala ya kisiasa kwa wasomaji na

sisi watafiti pia. Pasipo matumizi ya mbinu hizi ingekuwa kazi ngumu mno kwetu kupata masuala ya kisiasa yaliyowasilishwa katika dhumuni mahususi la kwanza la utafiti huu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHI, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Shaaban Robert ametunga kazi nyingi za fasihi za ushairi, riwaya na insha. Kazi hizi zina utajiri wa dhamira zenye mafunzo, maadili na nasaha nzuri kwa maendeleo ya taifa. Katika utafiti tumetumia riwaya zake mbili za *Kusadikika* na *Kufikirika* kutafiti masuala ya kisiasa katika riwaya hizo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, masuala ya kisiasa yanayosawiriwa katika riwaya hizo yametoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya siasa nchini Tanzania. Haya yamebainika kupitia madhumuni mahususi matatu yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu. Muhtasari wa kila dhumuni mahususi ni huu ufuatao.

## 5.1 Muhtasari wa Masuala ya Kisiasa katika Riwaya Zilizoteuliwa

Dhamira kuu zilizowasilishwa na Shaaban Robert katika riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika* ni uongozi katika jamii; uongozi mzuri, uongozi mbaya, utii wa sheria, masuala ya jinsia, kujifunza kutoka kwa watu wengine na amani, umoja na mshikamano. Tukianza na ile ya uongozi mzuri, Shaaban Robert anaonesha kuwa ipo haja ya msingi kwa serikali kuwajali wananchi wake kwa kuwashirikisha katika maamuzi yenye athari chanya na hasi kwa watu hao. Ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi huiwezesha serikali kupata mawazo na fikra nyingi zenye hazina ya mafanikio kutoka kwa wananchi hao. Pia, wananchi wanaposhirikishwa katika maamuzi ya mambo yanayowahusu hujiona kuwa ni wamiliki wa maamuzi hayo na kufanya kazi ya utekelezaji kuwa nyepesi. Serikali ya Tanzania imefuata maelekezo ya Shaaban Robert na kuamua kuwashirikisha wananchi wake katika ujenzi wa shule za sekondari kwa kila kata, mradi ambao umefanikiwa vizuri kabisa.

Kwa upande wa uongozi mbaya, Shaaban Robert anaonesha kuwa utawala usiokuwa na huruma kwa watu wake huchukiwa na watu hao. Anatoa mfano wa serikali ya Kikoloni ambayo ilipata utajiri mkubwa kwa kuwatumikisha wananchi wa Tanganyika kwa malipo kidogo na masaa mengi ya kazi. Serikali hiyo ya Kikoloni haikuwa na huruma kwa wananchi kwa sababu haikuwapatia huduma nzuri za kibinadamu kama mrejesho wa kazi nzuri waliyoifanya ya kuzalisha mali nyingi kwa ajili ya serikali ya Kikoloni. Serikali ya Tanganyika Huru iliamua kufanya kazi ya ziada kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za kibinadamu kama elimu, afya, maji, makazi, mavazi na chakula. Ilifanya hivyo kwa kuanzisha vijiji vya ujamaa na kujitegemea na katika kila kijiji kulikuwa na upatikanaji wa huduma muhimu za ustawi wa maisha ya binadamu (Nyerere, 1967). Haya ni mafunzo kutoka katika maandishi ya Shaaban Robert yaliyozitaka serikali na watawala wake kuwa na huruma kwa wananchi inaowaongoza.

Utii wa sheria ni chanzo cha utawala bora katika jamii. Shaaban Robert anaeleza kwamba, anayepaswa kutii sheria na mamlaka za nchi si mwananchi peke yake bali hata kiongozi. Imetokezea kuona baadhi ya viongozi kutaka kufanya mambo bila ya kuzingatia sheria za nchi ili kulinda masilahi yao. Majivuno na baadhi ya wajumbe wa baraza za Kusadikika ni miongoni mwa viongozi waliokuwa na hila ya kuvunja sheria kwa masilahi binafsi ya kuimarisha utawala wao hata kama ulikosea. Hii inaonekana pale Majivuno alipotaka Karama ahukumiwe kifungo kwa kuanzisha na kufundisha taaluma ya Uanasheria katika nchi ya Kusadikika. Hata hivyo, Mfalme wa nchi alikubaliana na maombi ya Karama ya kupewa muda wa siku sita kuwasilisha ushahidi wake mbele ya baraza hilo. Baada ya Karama kuwasilisha

ushahidi wake alikutwa hana hatia yoyote na kuachiwa huru. Mfalme alionesha mfano mzuri wa kutoa haki kwa raia wake. Nchini Tanzania kumekuwa na hali kama hiyo ambapo hakuna mtu anayehukumiwa kifungo kidogo au kikubwa bila kusikilizwa. Kiongozi na raia wote wameonesha utii wa sheria na mamlaka za nchi.

Jamii yoyote ile haiwezi kupata maendeleo kama haitahakikisha kuwa raia wake wote, wanaume kwa wanawake, wanashiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yao. Hili litafanikiwa kwa kushughulikia masuala ya jinsia katika jamii. Shaaban Robert anaona kuwa wanawake wamekuwa msitari wa mbele katika kufanya kazi za uzalishaji kwa taifa lakini mchango wao hauthaminiwi. Hauthaminiwi kwa sababu hakuna mrejesho wowote aupatao mwanamke kutokana na kazi anazofanya za kuzalishia familia na taifa. Wanaume ndio hunufaika zaidi na nguvu kazi ya wanawake na wanawake wanaendelea kuwa masikini. Serikali ya Tanzania imefanya jitihada kubwa ya kuhakikisha mchango wa wanawake katika maendeleo ya familia na taifa unathaminiwa kwa kuwapatia huduma bora za afya, ajira, mikopo midogomidogo, elimu ya ujasiriamali na nafasi za upendeleo katika vyombo vya maamuzi (Ngaiza, 2002). Pamoja na hatua za kuwapatia wanawake fursa sawa na wanaume bado kuna changamoto kadha wa kadha zinazohitaji kushughulikiwa.

Kudumisha amani, umoja na mshikamano ni vitu muhimu vilivyosisitizwa mno na Shaaban Robert. Kuwepo kwa amani katika jamii ndiko kunakotoa fursa ya kufanyika kwa shughuli mbalimbali za maendeleo. Amani ikikosekana inakuwa si rahisi kwa mtu yeyote kujishughulisha na kazi za uzalishaji mali au utoaji wa huduma za afya, elimu, usafiri, maji, umeme na nyinginezo. Sambamba na kuwepo kwa amani ni lazima pia wananchi wawe na umoja na mshikamano baina yao. Hii

itawafanya kuoneana huruma na kusaidiana katika raha na karaha. Serikali ya Tanzania imefanya jitihada kubwa ya kuhakikisha nchi inakuwa katika amani, umoja na mshikamano wakati wote. Hata hivyo, yapo matukio kadhaa ambayo yanaonesha uvunjifu wa amani nchini. Matukio hayo ni kama viongozi wa dini na watalii kumwagiwa tindikali huko Zanzibar, mauaji ya walemavu wa ngozi, milipuko ya mabomu Arusha na Zanzibar yaliyosababisha vifo vya watu kadhaa na kujeruhi wengine kadhaa. Jitihada za kupambana na matukio haya zimefanywa na zinaendelea kufanywa ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa kisiwa cha amani, umoja na mshikamano.

## 5.2 Muhtasari wa Mbinu za Kisanaa katika Riwaya Zilizoteuliwa

Utafiti huu umegundua kuwa masuala ya kisiasa yanawasilishwa na Shaaban Robert kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa. Hata hivyo, katika utafiti huu zimeteuliwa mbinu tano zilizotafitiwa na kuwasilishwa. Mbuni ya kwanza ni matumizi ya methali. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mbinu hii inasaidia wasomaji kuelewa dhamira zilizolengwa kwao na mtunzi kwa urahisi. Mtunzi ametumia mandhari ya nchi iliyo angani isiyokuwa na uhalisia katika maisha ya jamii ya ulimwengu unaofahamika. Matumizi ya mbinu hii yanawafanya wasomaji kuona kuwa kile kinachosemwa hutokea katika nchi ya *Kusadikika* na *Kufikirika*, kinatokea pia katika nchi wanazoishi. Hii ni kwa sababu wana matumizi ya methali kama hizo katika maisha yao ya kila siku.

Tashibiha zimetumika kutoa msisitizo juu ya dhamira za kisiasa katika *Kusadikika* na *Kufikirika*. Msisitizo uliotolewa ni ule wa kuonesha namna Majivuno alishikilia madaraka tangu akiwa kijana mdogo mpaka anazeeka bado tu anaendelea kutawala.

Katika jamii kadhaa duniani bado wapo viongozi wa aina hii ambao hujiona wao ndiyo wanaostahili kuwa viongozi na wengine hapana. Ametumia tashibiha ili kuwataka viongozi waliopo madarakani kutodhani kuwa wao ndiyo wao na hakuna mtu mwingine awezaye kuwa kiongozi. Uongozi ni dhamana na huwa una mwisho wake.

Mbinu nyingine iliyotumika kuwasilisha dhamira za kisiasa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* ni kejeli. Riwaya hizi ziliandikwa katika kipindi cha Ukoloni ambapo utawala huo ulikuwa ni wa kinyonyaji na dhuluma kwa wananchi. Shaaban Robert anatumia kejeli kuwapamba viongozi hasa Wafalme kuwa walikuwa ni watu Rahimu na karimu kwa wananchi wao. Ni jambo la kweli kwa baadhi ya Wafalme kuwa ni viongozi wenye huruma kwa watu wao lakini serikali ya Kikoloni nayo ilikuwa ikiongozwa na Malkia ambaye ni sawa na mfalme. Malkia huyo hakutenda kama vile alivyopaswa kuwatendea watu wake na badala yake aliwadhulumu watu wote katika makoloni. Shaaban Robert anapomtaja mfalme kuwa alikuwa ni mtu mwenye huruma kwa watu wake anamkejeli kwa sababu anafahamu kabisa hali haikuwa hivyo.

Mandhari ya kiuhalisiaajabu nayo imetumika kusawiri vilivyo masuala ya kisiasa katika jamii. Mandhari ya nchi iliyo angani imemuwezesha mtunzi kuwa na uhuru wa kueleza madhila yaliyokuwa yakifanywa na serikali ya Kikoloni kwa wananchi wa mataifa iliyoyatawala. Matumizi ya mandhari ya aina hii imeonesha ufundi wa kisanaa aliojaaliwa Shaaban Robert katika utunzi wake wa kazi za fasihi. Nchi inaelea angani lakini ina viongozi na wananchi wanaotenda mambo mbalimbali. Kupitia mandhari hii tumepata dhamira za uongozi mzuri na mbaya katika jamii, utii

wa sheria, kujifunza kutoka kwa wengine, masuala ya jinsia na amani, umoja na mshikamano katika jamii.

## 5.3 Hitimishi

Riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* zinatoa mchango muhimu wa namna bora ya kuelekeza utawala bora katika jamii. Riwaya hii imeandikwa katika mandhari dhahania isiyo na uhalisia hata kidogo lakini inasadifu hali halisi ya maisha ya jamii halisia ulimwenguni kote. Suala la uongozi mzuri kwa wananchi ni kitu muhimu mno katika kuleta maendeleo kwa wananchi hao. Riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* zinaeleza kuwa vitendo vya rushwa, dhuluma, ufisadi, uonevu, kutotiiwa kwa sheria na kutoshirikisha wananchi katika maamuzi yanayowahusu ni vyanzo vikubwa vya kuongeza umasikini katika jamii. Nchi za Kusadikika na Kufikirika zilikuwa na viongozi ambao walijali masilahi yao kuliko masilahi mapana ya jamii. Madhila haya yalifanywa na viongozi wa serikali ya Kikoloni dhidi ya raia wa nchi walizozitawala. Mambo haya bado yanaendelea kutokea hata katika jamii za leo ambapo viongozi ni watu tajiri sana na wananchi wa hali za chini ni masikini kupita kiasi.

Ushughulikiaji wa masuala ya kijinsia ni muhimu katika kuleta maendeleo kwa jamii. Katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* kunaonesha nafasi kubwa waliyonayo wanawake katika kuleta maendeleo kwa taifa. Wanawake ndio wazalishaji wakubwa wa bidhaa na huduma adhimu kwa mustakabali wa maisha ya mwanadamu. Jambo la kushangaza ni kuwa, wanawake wamekuwa wazalishaji tu na si walaji wa bidhaa na huduma katika jamii. Hii inatokana na kuwapo kwa mfumo dume ambao unampa mwanaume umiliki wa rasilimali na mwanamke akiwa ni

mtumishi tu katika rasilimali hizo. Kwa mfano, mwanaume ndiye anayemiliki shamba na mwanamke ndiye mfanyakazi mkuu katika shamba hilo. Mavuno yanayopatikana huwa mali ya mwanaume na si mwanamke kwa kuwa yeye si mmiliki wa shamba hilo. Hali hii huwafanya wanaume kutumia mali zilizozalishwa na mwanamke kwa masilahi binafsi na kuiacha familia ikiteseka katika mikono ya mwanamke (Koda, 2000). Kupitia riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* jamii inaaswa kuhakikisha kuwa inatoa nafasi sawa ya umiliki wa mali baina ya mwanamke na mwanaume kama njia sahihi ya kulileteа taifa maendeleo.

## 5.4 Mapendekezo

Sehemu hii inatoa mapendekezo katika maeneo yanayohusiana na mada ya utafiti.

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Serikali

Tunapendekeza kuwa serikali ifanye uamuzi mzito wa kuelekeza Wizara ya Elimu juu ya kutumika kwa vitabu vya Shaaban Robert katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu. Vitabu vya riwaya vya Shaaban Robert kama *Kusadikika* na *Kufikirika* vina utajiri mkubwa wa mambo mazuri ambayo yanapaswa kufahamika kwa vijana wadogo ili kujenga uzalendo kwa nchi yao. Iwapo itakuwa ni lazima kila mwanafunzi kusoma vitabu hivyo, hakuna shaka kuwa, uzalendo kwa taifa utakuwepo kwa vijana ambao ni taifa la kesho.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Wachapaji

Wachapaji wa vitabu ndio huwezesha jamii pana kupata nakala za kujisomea na kukuza maarifa yao. Tunawashauri wachapaji tafautitafauti wajitokeze kuchapa kazi za Shaabana Robert na kuziuza kwa bei nafuu ili kila msomaji aweze kununua nakala

yake. Katika miaka kama ishirini iliyopita, kazi za Shaaban Robert hazikuchapwa kwa sababu wachapaji hawakulipwa fedha walizokuwa wanadai. Hii ilifanya vijana wengi kushindwa kupata utajiri wa mafunzo kuhusu maisha kutoka katika kazi za Shaaban Robert.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Wasomaji

Tunapendekeza kuwa kila Mtanzania aone fahari kubwa kusoma kazi za riwaya za Shaaban Robert ili kupata maarifa mengi kuhusu maisha katika riwaya hizo.

### 5.4.4 Mapendekezo ya Utafiti wa Baadae

Tunapendekeza utafiti kama huu wa kuchunguza masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert ufanyike katika riwaya zake nyingine ambazo hazijashughulikiwa katika utafiti huo. Utafiti huu ukifanyika tutapata picha kamili ya masuala ya kisiasa katika riwaya hizo na kutoa mchango muhimu wa kujenga uzalendo kwa wananchi wa Tanzania.

Pia, tunapendekeza kuwa ufanyike utafiti ambao utachunguza matumizi ya mbinu za kisanaa katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert. Utafiti huu uchunguze mbinu za kisanaa kwa undani ili kuweza kutoa picha kamili kama kuna ukweli wowote kuwa mambo anayozungumza Shaaban Robert ni ya Kiuhalisiamazingaombwe na hayatekelezeki.

## MAREJELEO

Aronson, J. (1992), "A Pragmatic View of Thematic Analysis" in the *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Pp (37-73). Oro lando FL: Grune& Stratton.

Babbie, E. (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth

Bathes, R. (1994), *The Semiotic Challenge* Berkely: University of Califonia Press.

Bentoncini, E. (1980), "Two Contemporary Swahili Writers, katika *the East African Experience na Ulla Schild* (mha) Reiner Berlin.

Beja, S.K. (1988), "Maudhui ya Ujamaa katika Riwaya za Tanzania," Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Benner, P. (1985), "Quality of Life: A phenomeno logical perspective on explanation, prediction and Understading in Nursing Science", *Advanees in Nursing Science*, 8(1), 1-14.

Bogdan, R. (and Biklen, S.K. (1992), *Qualitative Research of Education: An introduction to Theory and Methods,* (end ed), Boston: Allyn and Bacon

Chandler, D. (1992), *Semiotics: The Basics* London, Routledge Press.

Chohen, L. et, al. (2000), *Research Methods in Education* ($5^{th}$ end) London:

Chuachua, R. (2008), "Taswira katika Riwaya za Shaaban Robert," Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro.

Chuachua, R. na Wenzake, (2009), "Shaaban Robert: Vita na Ukoloni," Katika *Mulika*, kur.148-155, TUKI.

Chuachua, R. (2011), *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*, Dar es Salaam: TATAKI.

Creswell, J.W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitatie, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.

John, L. (2007), *Critical Reading: A Guide.* In http://www. Brocku. Ca/English/jlge/criticalreadig. Html. Accesssed, 30th, October 2006

Kezilahabi, E. (1976), "Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya," Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1983), "Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi," katika, *Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namba 3*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 226-243.

Keys, B. na Wenzake (1989), "Four Faces of Fully Function Middle Manger; California Management Review; Vol. XXIV. No, 4 pp. 59-67.

Khamis, S.A.M. (2007), "Utandawazi au Utandawizi?: Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai," katika *Kiswahili*, Juzuu namba 70, Dar es Salaam: TUKI, Kur.47-66.

Koda, B. (2000), "The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District", Unpublished *Ph.D Thesis*, UDSM.

Kothari, C.R. (1992), *Reserch Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari, C.R. (2008), *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Leininger, M.M. (1985), "Ethnography and Ethnonursing: Model and Modes of Qualitative Data Analysis". In. M.M. Leininger (Ed.). *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Pp (37-73). Oro lando FL: Grune& Stratton

Mbatiah, A.M. (1999), "The Origion and Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania," Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mbughuni, P. (1978), "The Themes of a New Society in the Kiswahili Prose: From Oral to Written Literature," Katika *Kiswahili*, Juzuu Na. 48/2:21, TUKI.

Mlacha, S.A.K. (1987), "The Portrayal of Cultural Conflict in Kiswahili Prose Fiction; A Structual Study of the Novels of Euphrase Kezilabi" Tasnifu ya Uzamivu (Ph.D) University of London.

Mpangala, G.P. (1977), *Political and Social Development in Afrika* Dar es Salaam: DUP.

Mpangala, G.P. (2007), "The Role of Civil Society in the 2005 General Elections in Tanzania," In, Tanzania *Journal of Development Studies*, Vol. 7, No. 2 Pp. 1-18. Dar es Salaam: IDS.

Msokile, M. (1993), *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*, Dar es Salaam: DUP.

Mong'eri, O.B. (2000), "Utetetezi wa Maadili katika Fasihi: Nadharia ya Shaaban Robert," Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Newman, W.L. na Wenzake, (2006), *Social Research*. Sixth Edition, Boston: Pearson.

Ngaiza, M.K. (2002), "Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study." Unpublished, *Ph.D. Thesis*, UDSM.

Njogu, K. na Rocha. C. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.

Nyerere, J.K. (1967), *Ujamaa: The Basis of African Socialism*, Dar es Salaam: Tanganyika Standard.

Ohly, R. (1981) *Aggressive Prose*. Dar es Salaam: TUKI.

Omary, M. (2011), "Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Euphrase Kezilahabi," Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Omary, M. (2012), "Prospects and Challenges of Using Ward Health Committes for Improving Public Health at Ward Level in Tanzania: The Case of

Kinondoni Municipality," Un published M.A Disertation, University of Dar es Salaam.

Robert, S. (1951), *Kusadikika*. London: Nelson.

Robert, S. (1967), *Kufikirika*. Nairobi: OUP.

Robert, S. (1968), *Siku ya Watenzi Wote*. London: Nelson.

Robert, S. (1968), *Utubora Mkulima*, Nairobi: Nelson.

Robert, S. (2003), *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robson, C. (2007), *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Sheglov, Y. (1976), *Mordern Literature in Tropical African Languages*, Moscow: Nauka.

Sengo, T.S.Y. (1975), *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake*, Nairobi: Foundation Books.

Senkoro, F.E.M.K. (1976), "Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili," Katika Kiswahili, kur. 74-80, TUKI.

Senkoro, F.M.E.K. (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.

Taib, A.H. (2008), "Mkabala wa Kiislamu katika Uchanganuzi na uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili," CHAKAMA, kur. 133-141.

Taib, A.H. (2009), "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi," katika Mulika, kur. 130-147. TUKI.

Tangoh, M., (2008), Shaaban Robert: Mtetezi wa Mwanamke, Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Cha Waislamu Morogoro.

Taylor, S.J. & Bogdan. R. (1984), *Introduction to Qualitative Research Methods: The Search for Meanings*. New York: John Wiley& Sons.

Wafula, R.M. (1989), "The Use of Allegory in Shaaban Robert's Prose works," Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Yin, R.K. (1994), *Case Study Research: Design ad Methods*, (2nd eds. Thousands Oaks Calif: SAGE publishers.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATISHO NAMBA 1: Dodoso la Usaili kwa Jamaa wa Shaaban Robert

### A: Utangulizi

Mimi ninaitwa Bibiana Ambrose Massawe mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili wa sanaa katika fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya Utafiti wenye anuani isemayo **Kuchunguza Masuala ya Kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert: *Kusadikika* na *Kufikirika***. Ili niweze kupata data za kuweza kukamilisha utafiti huu nimeandaa dodoso hili ambalo ndani yake kuna maswali yaliyolengwa kwako na ninaomba nikufanyie usaili.

### B: Taarifa Binafsi za Msailiwa

Jina………………………………

Elimu…………………………….

Umri……………………………..

Kazi……………………………...

Mahusiano na Shaaban Robert……………………………………………

### C: Maswali

1. Naomba unieleze vile ulivyopata kumfahamu Shaaban Robert.
2. Shaaban Robert anasifika sana kwa mambo yapi?
3. Shaaban Robert alikuwa mpenzi wa mambo gani?
4. Ni mambo gani ambayo aliyachukia sana?
5. Tutajie Kazi za riwaya alizopata kuandika Shaaban Robert.
6. Ni kazi ipi ambayo wewe binafsi unaipenda sana? Kwa nini unaipenda kazi hiyo?

**Asante Sana Kwa Ushirikiano Wako**